# Nipashe

Jumatatu Agosti 17, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580312

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Mwenyekiti adakwa madai ya kuomba rushwa ya ngono

UKURASA 2



Nipashe Spotika

MABEKI WA5 WALIOFUNGA MABAO MENGI MSIMU HUU

SERGIO RAMOS

UKURASA 11

# Ni wiki ya lala salama

• **Hatima** wagombea ubunge CCM kujulikana, Polepole asema waliotoa rushwa watashikishwa adabu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**KITUO UBUNGO KUHAMIA MBEZI LUIS OKTOBA 15**

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, amemuagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Spora...

**UKURASA WA 4**

**PM AKARIBISHA UWEKEZAJI MPYA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa rai kwa wawekezaji kuchangamkie fursa nchini kwa kuangalia maeneo mazuri ya kufanya uwekezaji mpya...


## BAVICHA yapitisha mambo 11 ya kisera

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (wa pili kushoto), akiongoza kilele cha mbio za hisani zilizoandaliwa na Benki ya CRDB (CRDB Marathon 2020) jana, zilizomshirikisha pia Rais mstaafu Jakaya Kikwete (kulia) kwa ajili ya kutafuta fedha za kuwasaidia watoto wenye matatizo ya moyo wanaohitaji upasuaji katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto). **Habari Uk. 5. PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# ACT yatangaza wagombea wake ubunge, uwakilishi

UKURASA 2


**MICHEZO** NAMUNGO YAMNASA BEKI WA YANGA UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# M/kiti mbaroni kwa tuhuma rushwa ngono

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, inamshikilia Mwenyekiti wa Kijiji cha Kimana, Wilson Ngolanya (63), kwa tuhuma za rushwa ya ngono.

Taarifa za kukamatwa kwa mwenyekiti huyo zilitolewa jana na Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Holle Makungu, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema Ngolanya alikamatwa Agosti 15, majira ya jioni katika nyumba ya kulala wageni iliyopo mjini Kibaya akiwa utupu huku akiwa amevalia kondomu tayari kwa kutekeleza uhalifu huo.

"Awali tulipokea taarifa toka kwa mlalamikaji binti wa miaka 23 (jina limehifadhiwa), akimtuhumu mwenyekiti huyo wa kijiji kwa kuomba rushwa ya ngono," alisema Makungu.

Alisema uchunguzi wao ulibaini Ngolanya alikuwa akiomba rushwa ya ngono ili aweze kumsaidia mlalamikaji kuwaondoa wavamizi watatu kwenye shamba lililokuwa likimilikiwa na baba wa binti huyo ambaye kwa sasa ni marehemu. "Uchunguzi unaonyesha kuwa Ngolanya anafahamu kuwa shamba hilo lilikuwa la marehemu baba wa binti huyo," alisema.

Makungu alisema mwenyekiti huyo alimtaka binti huyo ampe rushwa ya ngono ili aweze kuwaondoa wavamizi hao katika shamba la marehemu baba yake.

"Binti huyo baada ya kuona usumbufu unazidi alitoa taarifa TAKUKURU na baada ya kujiridhisha na uchunguzi wa awali makachero wetu waliandaa mtego uliofanya kukamatwa kwa mtuhumiwa," alifafanua.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 kinasema, mtu yeyote aliye kwenye mamlaka au uongozi ambaye kwa kutumia mamlaka au cheo alichonacho akilazimisha sharti la rushwa ya ngono ili aweze kumpa mtu yeyote ajira. Kifungu hiki na sheria inakataza kupandishwa cheo, kumpa haki stahiki, upendeleo au unafuu asiostahili anakuwa ametenda kosa la rushwa ya ngono na ikithibitika adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiweka jiwe la msingi kiwanda cha samani kinachomilikiwa na Kampuni ya ORASCOM Construction and Engineering katika Kijiji cha Namkonjera wilayani Raungwa mkoani Lindi jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya ORASCOM, Magira Magoma Magesa. Habari Uk. 4. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Ni wiki ya lala salama

**Na Mwandishi Wetu**

NI wiki ya lala salama. Ndivyo unavyoweza kusema kwa wagombea urais wanaosaka wadhamini katika mikoa mbalimbali nchini, na kurejesha fomu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na wagombea ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanaosubiri kujua hatima yao.

Wagombea wa urais wa vyama 16 walishachukua fomu na wanatembea katika mikoa 10 ya Tanzania Bara na Visiwani kusaka wadhamini 2,000, kila mkoa ukitakiwa kutoa wadhamini 200.

NEC imesema Agosti 25, mwaka huu itakuwa ndiyo siku ya uteuzi wa wagombea urais.

**WAGOMBEA UBUNGE CCM**

Ni wiki ngumu kwa wagombea wa CCM, kwa kuwa Kamati Kuu ya chama hicho, itapitia jina moja moja la waliomba ridhaa ya kupitishwa na chama hicho kupeperusha bendera kwenye ubunge.

Tayari chama hicho kimewatahadharisha wagombea waliovunja kanuni, taratibu na katiba ya CCM kwa kutoa rushwa, kuandaa maandamano, kushangilia baada ya kushinda na nyinginezo kwamba watawashughulikia ipasavyo.

Kwa upande wa CHADEMA, imeshatangaza wagombea ubunge kwa kila jimbo na wameshaanza kuchukua fomu za kugombea ubunge kutoka kwa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo.

Akizungumza na Nipashe, Msemaji wa CHADEMA, Tumaini Makene, alisema mgombea urais wao, Tundu Lissu, ataanza ziara ya kusaka wadhamini katika mikoa ya kusini na baadaye Zanzibar.

Vilevile, alidai chama kimebaini kuwapo mkakati wa kupora fomu za wagombea ubunge, huku akitolea mfano wa tukio la mgombea ubunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi, kukamatwa na kuachiwa na kuchomwa kwa ofisi za CHADEMA Kanda ya Kaskazini ambazo zinahifadhi fomu za wagombea udiwani na ubunge.

"Tunafuatilia kwa karibu sana kuhakikisha wagombea wetu wanajaza fomu kwa usahihi, anarejesha, usalama wao na usalama wa fomu. Watasindikizwa na wanachama wetu ili kukabiliana na mbinu ovu iliyoanza kujitokeza," alifafanua.

**ACT-WAZALENDO**

Chama cha ACT-Wazalendo, kimetangaza awamu ya kwanza ya majina ya wagombea ubunge katika baadhi ya majimbo nchini na wataanza kuchukua fomu.

**NCCR NA CUF**

Chama cha NCCR-Mageuzi na Chama cha Wananchi (CUF) vinatarajiwa kutangaza majina ya wagombea ubunge wa majimbo.

**NDANI YA CCM**

Kwa sasa wagombea waliotuhumiwa kwa rushwa wako tumbo jopo kutokana na kauli iliyotolewa na chama hicho kuwa waliojihusisha na rushwa watakatwa.

Ndani ya CCM kiu kubwa iko kwa nafasi ya ubunge ambazo zilighubikwa na vimbwanga vingi ikiwamo utitiri wa wagombea, rushwa na vituko vya kila aina.

Ngazi mbalimbali ndani ya CCM zimemaliza kupata majina ya wagombea ambazo ni Jumuiya ya (UVCCM), Jumuiya ya Wanawake (UWT) na Jumuiya ya Wazazi. Baadhi ya sauti na video za baadhi ya wagombea za ugawaji fedha na zawadi kwa wajumbe wa mikutano wa jimbo ambao walipiga kura zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi wakichukuliwa hatua na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Baadhi ya wagombea walikamatwa kabla ya kusambaza zawadi na fedha aliokuwa nao na kuishia mikononi mwa TAKUKURU, na waliendelea na harakati za kuwania nafasi hizo na sasa panga la CCM linasubiriwa.

**POLEPOLE: TUTAWAFUNDISHA ADABU**

Mwishoni mwa wiki, akizungumza katika uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Hamphrey Polepole, alisema wiki hii mbivu na mbichi zitajulikana kwa kuwa vikao vitafanya maamuzi ya wagombea ubunge.

"Tunaenda kuweka mambo sawa, naenda Dodoma usiku huu (juzi), wana-CCM waliomba dhamana CCM waendelee kuwa watulivu, wanyenyekevu, waaminifu, watiifu," alisema.

"Wale ambao hawakutoa rushwa, wale waliofuata katiba na kanuni za chama wawe na amani. Wale waliovunja utaratibu, wavurugaji tutawafundisha adabu wakati huu."

Polepole alisema Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa inasimamia utaratibu na inafuatilia hadi ngazi ya tawi.

"Taarifa za watu zinajulikana, ulitoa rushwa siku fulani muda fulani tunazo, tuna nyaraka kubwa na tunazisoma, ili kuondokana na watu wanaovunja utaratibu wa chama chetu. TAKUKURU imefanya kazi nzuri waliokatamatwa na jinai wafungwe ila wale waliotuhumiwa tutashughulika nao," alisema.

Wiki iliyopita, TAKUKURU ilisema kuwa imekabidhi ripoti CCM, ili ishughulike na watu waliotuhumiwa au kuthibitika kuhusika na rushwa.


**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**ABEL PAUL MWAKALINDILE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **Toyota BREVIS** yenye namba za usajili **T 777 DDN.** Chassis no. **JCG100054153,** Engine no. **1J2054153.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/43/18/2020.**



**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T. LTD &COURT BROKER**

**MNADA WA HADHARA**

UTAFANYIKA TAREHE **29/08/2020 SAA 4: ASUBUHI,** KWA IDHINI YA MAHAKAMA YA MWANZO YA CHAMWINO IKULU KESI NAMBA 18 YA MWAKA 2019. TUTAUZA NYUMBA ILIYOPO MSANGA CHAMWINO IKULU KUFIDIA DENI ANALODAIWA.

**MAWASILIANO PIGA NO. 0713913150.**


# ACT yaanika wagombea wake ubunge, uwakilishi

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetangaza majina ya wagombea wake wa ubunge na uwakilishi kwa awamu ya kwanza, huku waliokuwa vigogo katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wakipewa nafasi ya kugombea kupitia chama hicho.

Akitangaza orodha hiyo, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema jana kuwa chama hicho kimeshakamilisha maandalizi yote muhimu kwa ajili ya kuingia katika uchaguzi huo.

Baadhi ya wagombea waliotangazwa ni pamoja na Saed Kubenea, ambaye anagombea Jimbo la Kinondoni, Mbarala Maharagande anagombea Jimbo la Segerea wakati Kigoma Mjini akirejea Kiongoni Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe. Ubungo ni Renatus Pamba, Ukonga Webiro Wassira, Kigamboni Mwanaisha Mndeme, Ilala Hussein Abdallah, Lindi Mjini Isihaka Mchinjita, Kilwa Kusini Seleman Bungara na Kilwa Kaskazini Shaweji Mketo.

Wengine ni Jimbo la Kibamba, Moses Ndonde , Mbagala -Kondo Bungo, Tanga Mjini -Rashid Jumbe Hamza, Pangani- Faraji Msagati, Kigoma Kaskazini Swage Zahir, Buyungu -Mtondo Balele, Kigoma Kusini- Said Bakema na Kasulu Mjini- Hamza Mtunu. Kwa upande wa wawakilishi ni Bumbwini -Zahran Mshamba, Donge -Pavu Juma, Mahonda -Thuwaiba Hussein, Kikwajuni- Rashid Rashid, Kwahani-Omar Makame, Mpendae -Ali Hamad ,Malindi -Ismail Jussa, Jang'ombe -Abdallah Ali na Chumbuni-Khamis Mohammed.

Wengine ni Jimbo la Konde- Issa Juma, Micheweni- Subeit Faki, Tumbe-Mmanga Hemed, Chaani-Khatib Juma, Kijini- Haji Makame, Nungwi -Hassan Masoud, Kiembe Samaki -Ali Suleiman, Mwanakwerekwe- Abdillah Hassan na Chwaka-Thani Ame.

## HABARI KITAIFA

# Kituo Ubungo kuhamia Mbezi Luis Oktoba 15

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, amemwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Spora Liana, kuhakikisha mabasi yaendayo mikoani yanahamia katika kituo kipya cha mabasi Mbezi Luis, kabla ya Oktoba 15, mwaka huu.

Nyamhanga alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembea kituo hicho cha mabasi, kwa ajili ya kukagua maendeleo ya mradi huo ambao ujenzi wake umefikia asilimia 77.

Alisema Halmashauri ya Jiji hilo, inapaswa kuhakikisha ujenzi huo unakamilika katika muda uliopangwa ili kuanza kwa utekelezaji kama ambavyo imepangwa.

"Mkurugenzi hakikisha mabasi yote ya mikoani yanahamia hapa kabla ya Oktoba 15 muda ambao mmepanga mradi uwe umekamilika," alisema Nyamhanga. Alisema mabasi hayo yanapaswa kuhama kutoka kituo cha mabasi Ubungo ili kupisha eneo hilo kwa ajili ya kuwa Karakana Kuu ya Mabasi ya Yaendayo Haraka.

Alisema eneo hilo lilipaswa kuwa limeshakuwa wazi kwa ajili ya kuwa karakana ya mabasi hayo, lakini kutokakamilika kwa mradi huo wa kituo cha mabasi cha Mbezi Luis kwa wakati kumesababisha kutotekelezwa kwa mpango huo.

"Nimewaagiza na naendelea kuagiza kuwa, miradi yote ya kimkakati kama hiki kituo cha mabasi naomba niwe napewa ripoti ya maendeleo yake kila mwezi," alisema Nyamhanga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa jiji hilo, Liana aliahidi kuwa mradi huo utakuwa umekamilika Oktoba mwaka huu na matarajio yao kuhakikisha mabasi yote yanahamia katika kituo hicho kabla ya Oktoba 15, kama ambavyo wameagizwa na Katibu Mkuu. Alisema mradi huo unagharimu Sh. bilioni 50.94, na kwamba utakapokamilika unatarajia kuliingizia jiji hilo mapato ya Sh. bilioni 7.2 kwa mwezi.

Alisema hadi sasa katika mradi huo wameshatumia shilingi bilioni 20.46, na kwamba wanaweza kutumia chini ya gharama zilizopangwa na fedha zitakazobaki watazitumia katika shughuli nyingine za kuboresha kituo hicho.

Liana alisema mradi huo ulitakiwa uwe umekamilika kabla ya Julai mwaka huu, lakini umechelewa kwa sababu ya kuwapo kwa ugonjwa wa COVID-19 na uzembe wa mkandarasi ambaye hata, hivyo wameshambadilisha.

# BAVICHA yapitisha mambo 11 ya kisera

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

BARAZA la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), limepitisha sera yao ambayo ina mambo 11 ikiwamo vijana wenye miaka 30 kugombea urais.

Aidha, vijana wenye umri wa miaka 18 waruhusiwe kugombea udiwani na ubunge, kwa lengo la kuleta mabadiliko nchini na uzalendo.

Akiwasilisha sera hiyo, Ofisa Uchaguzi CHADEMA Makao Makuu, Alphonce Lusako, wakati wa kongamano la BAVICHA mkoani Mwanza, alisema katiba ya nchi kijana ni mwenye umri wa miaka 18 hadi 20 amepewa haki ya kupiga kura tu.

Alisema hana haki ya kuchaguliwa kwa upande wa urais kwa sababu kuwa hajafikisha umri wa miaka 40 na kuendelea, na kwamba wakati umefika wa kufanya mabadiliko.

"Kwa kulitambua hitaji hili la msingi la vijana kushiriki katika uongozi wa juu wa taifa, tutaishawishi serikali ya CHADEMA kufanya marekebisho ya katiba ili kurekebisha sharti la umri wa kugombea nafasi hizo," alisema Lusako.

Alisema ni mara ya kwanza BAVICHA kuandaa sera na kwamba chama kitakapochokuwa dola watakuwa na uwezo wa kukishauri nini kifanyike kwa vijana.

Mambo mengine yaliyopo ni elimu na mafunzo kwa vijana, fursa za ajira kwa vijana umiliki wa uchumi na kwamba kwa sasa asilimia kubwa ya wananchi ni vijana ambao umiliki wao ni mdogo, ukuzaji wa vipaji vya michezo na sanaa, afya kwa vijana .

Mengine ni ushiriki wa vijana katika siasa, mawasiliano kama fursa ya kiuchumi kwa vijana, kilimo kama msingi wa uchumi kwa vijana kwani chama hicho kitahakikisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakati.

Jumuiya ya kimataifa, mazingira na kusimamia haki za binadamu sambamba na kuanzisha utaratibu wa wafungwa kupiga kura.

"CHADEMA ikishika dola matukio yote ukiukwaji wa haki za binadamu, vifo vyote vilivyotokea vya kisiasa bila ya ubaguzi huyu ni wa CCM ama CHADEMA yatachunguzwa ili waliohusika wanachukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Akizindua kongamano hilo, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema maeneo mengi nchini wagombea wa chama hicho wamechukua fomu.

"Tunaomba zoezi la upigaji kura lisianze mpaka mawakala wetu wawapo ndani, silaha yetu ni kadi za kupiga kura, tunahitaji nguvu ya umma na maombi haki yetu ya kugombea... tutaipata kwenye uchaguzi huu japokuwa mimi sitogombea, lakini kwa wale waliogombea tutaitafuta haki yao tutaidai kwa kila njia hadi ipatikane," alifafanua.

Naye Mwenyekiti wa BAVICHA, John Pambalu, alisema nakala za sera hiyo zitasambazwa katika maeneo mbalimbali yakiwamo vituo vya bodaboda, saluni, gereji ili kuleta hamasa na kutambua lengo halisi la sera hizo na pia watambue wajibu uliopo ni kutekeleza wajibu wa kizazi ama kuusaliti.

Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, John Heche, aliwapongeza BAVICHA kwa hatua hiyo, na kuwa nchi ni mali ya Watanzania, hivyo wakishika dola watayatekeleza yote waliopaswa.

Aliongeza kuwa changamoto kubwa ya vijana ni ajira kwani vyuo vikuu vya kati, shule za msingi na sekondari vimekuwa vikizalisha vijana wengi na wanaingiza kwenye soko la ajira bila kuwapo ajira zenyewe na kuwa hiyo inatokana na kutokuwapo kwa mpango madhubuti wa taifa kukabiliana na adha hiyo.




# Walioshtakiwa kuua askari waachiwa huru

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma, imewaachia huru washtakiwa 11 waliokuwa wakikabiliwa na kosa la kuua kwa kukusudia askari wawili wa Jeshi la Polisi na kukata sehemu za siri za mmoja wa askari hao katika mapigano yaliyotokea wakati wa kuwaondoa wananchi waliovamia eneo la Hifadhi ya Ranchi za Taifa (NARCO), wilayani Uvinza.

Hukumu hiyo ilisomwa Ijumaa (Agosti 14), na kesi hiyo ilihusu tukio lililotokea Oktoba, mwaka 2018, wakati wananchi karibu 1,000 walipojiunga kupambana na askari wakiwa na silaha za jadi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Ilvi Mgeta, alisema sababu za kuwaachia huru ni ushahidi alioutoa daktari wa Kituo cha Afya cha Lugufu, aliye wahudumia baadhi ya washtakiwa na kueleza kuwa risasi walizopigwa zilipita juu ya ngozi wakati washtakiwa wana makovu makubwa yanayoonyesha risasi zilipita upande mmoja na kutokea mwingine tofauti na shahidi alivyoeleza.

"Tunashindwa kuelewa kwa nini shahidi huyu alitoa ushahidi wenye nia ya kuidanganya mahakama wakati akiwa anajua ukweli ni ushahidi wa askari walioeleza kuwapo katika mapigano hayo."

Ushahidi mwingine ulioelezwa kuwa dhaifu ni wa askari walioeleza kushiriki operesheni hiyo kuwa walipambana na wananchi hao uso kwa uso na kufanikiwa kuwapiga risasi wakati wa mapigano, wakati makovu ya risasi hizo kwa watu 10 kati ya 11 walioshtakiwa, yakionyesha kuwa walipigwa upande wa nyuma na kutokea mbele hivyo wapigaji wa risasi hizo hawakuweza kuwaona uso kwa uso washtakiwa.

Pia, Jaji alisema gwaride la utambuzi halikufuata misingi ya sheria kwa kuwa mmoja wa washtakiwa alieleza kuwekwa kwenye mstari akiwa peku na wengine wakiwa na nguo zilizo jaa damu kutokana na majeraha ya risasi, hivyo kurahisisha kutajwa kuwa walihusika na mauaji hayo.

Kadhalika, alisema ushahidi wa aliyeshuhudia gwaride la utambuzi kuiambia mahakama kuwa hakuwaona washtakiwa hao katika gwaride la utambuzi pamoja na maelezo ya onyo yaliyoelezwa kuandikwa na washtakiwa, ambayo wote waliyakana mahakamani kuwa sio yao pamoja na kukamatwa eneo tofauti na tukio lilipotokea katika maeneo tofauti.

Baada ya Jaji Mgeta kupitia uchambuzi wa hoja za pande zote mbili za upande wa Jamhuri uliowakilishwa na Happyness Mayunga, Shaban Masanja na Riziki Matitu na upande wa utetezi ukiwakilishwa na Wakili Sadick Aliki, Kagashe Rweyumamu na Eliuta Kiviylo, alisema kwa kuzingatia uhalisia wa ushahidi uliowasilishwa mahakamani hapo kuonyesha kuwa na taarifa zinazopingana, ushahidi huo ni dhaifu na hauwezi kuwatia hatiani washtakiwa hao na mahakama hiyo imeamua kuwaachia huru washtakiwa wote 11.

Askari waliopoteza maisha kwenye tukio hilo ni Inspekta Ramadhani Mdimu na Koplo Mohamed Nzengohuku. Washtakiwa 11 waliochiwa huru ni Gelya Gisega, Jumanne Jackson, Nkono Mwandu, Shishi George, Masanja John, Hamis Masalu, Walwa Malongo, Makenzi Lukelesha, Masalu Inambali, Petro Bucheyeki na Charles Maduhu.



Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, akizungumza na wanafunzi ambao ni wanachama wa Klabu ya Kodi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDTA) mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## TAKUKURU yamuhoji mfanyabiashara bilionea

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), inamshikilia mfanyabiashara na mmiliki wa kampuni ya White Star Investment ya jijini Dar es Salaam.

Mfanyabiashara huyo anahojiwa kwa madai ya kuhusika na ukwepaji kodi, udanganyifu na utakatishaji fedha haramu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, mfanyabiashara huyo ni Taalib Mbowe, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo.

Alisema kampuni hiyo hujishughulisha na biashara ya usafirishaji ndani na nje ya nchi kwa kutumia malori.

Wakati huo huo, TAKUKURU inachunguza umiliki wa vichwa vya malori zaidi ya 100 vinavyomilikiwa na mfanyabiashara huyo.

"Pia tunachunguza mkopo wake wa zaidi ya Dola za Marekani 3,000,000 (Sh. bilioni 6.3) kutoka Benki ya Barclays pamoja na Dola za Marekani 540,000 (Sh. bilioni 1.1) kutoka benki ya Equity," alifafanua.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, uchunguzi ukikamilika na kuthibitisha tuhuma hizo, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

# Waziri Mkuu Majaliwa akaribisha uwekezaji mpya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa rai kwa wawekezaji kuchangamkie fursa nchini kwa kuangalia maeneo mazuri ya kufanya uwekezaji mpya au kupanua uwekezaji wao.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wakazi wa Namichiga, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi, waliohudhuria uwekaji wa jiwe la msingi kwenye kiwanda cha samani cha Saw Mill and Furniture Processing Industry na kisha kukagua eneo la ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho wilayani humo.

Waziri Mkuu alisema hicho ni kiwanda cha kwanza kujengwa Ruangwa na kuwataka wakazi wa Namkonjera na vijiji vya jirani wapime ardhi yao ili watu wanunue viwanja na kuanza kujenga.

"Kujengwa kwa kiwanda cha kutengeneza samani na baadaye kiwanda cha kubangua korosho, kutahamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo na misitu pamoja na kuimarisha mnyororo wake wa thamani. Endapo mtajipanga vizuri kwa kujenga viwanda vya kuongeza thamani kwenye zao la korosho, wilaya hii itakuwa kinara kwenye uzalishaji wa zao hilo," alisema.

"Kwa upande wa viwanda, tusiishie tu kwenye korosho, tuone pia namna ya kuwa na viwanda vya kuchakata ufuta, mbaazi na mazao mengine yanalimwa kwa wingi kwenye maeneo yetu ili kijihakikishia soko na upatikanaji wa ajira."

Alisema uwekezaji huo unaofanyika sasa, unakwenda sambamba na azma ya serikali ya kuanzisha na kuendeleza viwanda ili kukuza uchumi, kuleta maendeleo endelevu, kuongeza ajira na kupunguza umaskini kwa Watanzania wote.

Akifafanua kuhusu ujenzi wa viwanda nchini kote, Waziri Mkuu alisema kuimarika kwa uzalishaji hususan kupitia ujenzi wa viwanda, kumekuwa chachu ya upatikanaji wa huduma hususan kufuatia kuimarika kwa mapato ya serikali na kutengeneza ajira kwa Watanzania.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka mitano, serikali imefanikiwa kuimarisha sekta za kiuchumi na uzalishaji ikiwamo viwanda na biashara. "Katika kipindi hicho jumla ya viwanda vipya 8,477 vimejengwa na kuchangia kuzalisha ajira mpya 482,601," alisema.

Akizungumzia mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa, Waziri Mkuu alisema sekta hiyo imeendelea kukua mwaka hadi mwaka na kwa mwaka 2019 ilikua kwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na 8.05 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 0.45.2

"Mchango huo unakwenda sambamba na kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

Kwa mfano, mwaka 2019 bidhaa za viwanda zilikuwa na thamani ya Sh. trilioni 10.2 ikilinganishwa na Sh. trilioni 9.6 mwaka 2018 sawa na ukuaji wa asilimia 5.8," alisema.

"Maendeleo ya uwekezaji katika sekta ya viwanda tunayoyashuhudia hivi sasa hapa nchini, yameongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo za chuma, saruji, vigae, nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi, kusindika nyama, chakula, mboga na matunda, maziwa, mafuta ya kula, sukari, vifungashio, mbolea, dawa za binadamu, sabuni na sigara pamoja na ubanguaji wa korosho.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba, alisema uwekaji wa jiwe la msingi katika kiwanda hicho cha kutengeneza samani, ni matokeo ya msisitizo wa Rais Dk. John Magufuli na usimamizi wa karibu wa Waziri Mkuu mwenyewe kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Alisema serikali imepania kuongeza uzalishaji wa zao la korosho ifikapo mwaka 2025. "Wenye viwanda vyote vya korosho, nawahakikishieni kwamba tutakuwa na malighafi za kutosha, tumepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 300,000 hadi tani milioni moja ifikapo mwaka 2025," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hashim Mgandilwa, alisema anawashukuru na kuwapongeza Orascom kwa uamuzi wao wa kujenga kiwanda cha samani na cha kubangua korosho kwani utakuwa na manufaa ya kiuchumi na kielimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Magira Masegesa, alisema kiwanda hicho kinamilikiwa na kampuni ya wazawa ya Orascom Construction and Engineering Company (T) Ltd ikishirikiana na kampuni tanzu ya Yukos Enterprises yenye makao makuu jijini Dar es Salaam na kimeajiri wafanyakazi 150 ambao wanatengeneza samani zenye ubora kwa bei nafuu.

# Walimu wapatiwa hati 315 za ardhi

**Na Munir Shemweta,**
MWANZA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ametoa hati 315 za ardhi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza.

Utoaji wa hati hizo ni juhudi za serikali kuhakikisha walimu wa manispaa hiyo wanamilikishwa ardhi kwa gharama nafuu.

Walimu waliopatiwa hati za viwanja ni sehemu ya walimu 525 walioomba kupatiwa viwanja katika eneo la Nyamiswi Manispaa ya Ilemela, ambapo wengine walishindwa kukamilisha malipo ya viwanja hivyo.

Akizungumza wakati wa kugawa hati hizo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari za Manispaa ya Ilemela, Mabula aliwataka kuzitumia hati hizo kwa shughuli za maendeleo.

Kwa mujibu wa Mabula, kilichofanyika kwa walimu wa Manispaa ya Ilemela ni juhudi za Rais John Magufuli kutaka kila mwenye ardhi awe na umiliki ili kujua mipaka yake na kupata hati kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi na wakati huo kuitumia hati kwa shughuli za maendeleo.

Aliwaasa walimu kutumia benki hususan Benki ya NMB kuomba mikopo ya ujenzi wa nyumba, ili kuwezesha eneo walilopata kwenda kwa kasi hasa ikizingatiwa eneo hilo limepakana na eneo la Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo cha Afya na Hospitali ya Wilaya ya Ilemela na kubainisha kuwa eneo hilo ni zuri na hata kama walimu hao hawatakaa wanaweza kupangisha na kuingiza fedha kidogo kidogo.

Katibu wa Kamati ya mradi wa viwanja vya walimu katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Albert Mahuyu, alisema wamefanikiwa upimaji viwanja 525 na kuingiza kiasi cha shilingi milioni 404.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, alisema benki yake iko tayari kutoa mikopo kwa walimu na kubainisha mikopo inayotolewa na benki hiyo kuwa ni ile ya kununua, kuezeka na kumalizia nyumba pamoja na mkopo wa kurudishiwa fedha uliyojengea nyumba na mikopo iko hadi ya shilingi milioni 200 na unarejesha kidogokidogo kwa takriban miaka mitano.

# Tishio corona lilivyoathiri usalama wa chakula SADC

**Na Mwandishi Wetu**

JANGA la corona limesababisha uhaba na usalama wa chakula kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupungua, hali inayotishia ustawi wa wananchi wake.

Akiwasilisha mada wakati wa kikao cha pamoja baina ya waandishi wa habari, mashirika yasiyo ya kiserikali na wataalamu mbalimbali kujadili namna ya kushiriki katika masuala ya viwanda, kilimo na biashara, mshauri elekezi, Martin Muchero, alisema hali hiyo inatokana na ripoti ya ufuatiliaji ya mwaka huu.

Mkutano huo uliandaliwa na Jukwaa la Wakulima Wadogo wa Afrika Mashariki na Kusini (ESAFF), linalofanya kazi katika nchi 16, kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Ujerumani (GIZ) na Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema waathirika wengi wako vijijini na nchi zitakazoathirika zaidi ni Afrika Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya (DRC), na kwamba jumla ya watu 44,799,942 katika nchi wanachama waathirika.

Michero alitaja idadi ya walioathirika na usalama wa chakula ni Afrika Kusini (13,600,000), DRC (13,141,056), Angola (1,051,800), Botswana (38,300), Eswatini (366,261), Lesotho (433,000), Madagascar (554,000).

Nchi nyingine ni Malawi (2,700,000), Msumbiji (2,013,035), Namibia (354,438), Tanzania (488,661), Zambia (2,330,182) na Zimbabwe (7,729,209).

Aidha, katika nchi zote Tanzania ina hali nzuri kwa kuwa idadi ya walioathiriwa na usalama wa chakula ni asilimia moja, ikifuatiwa na Magadascar yenye asilimia tatu na Botswana asilimia sita.

Kuhusu mfuko wa maendeleo wa SADC, hadi sasa ni nchi saba pekee zimesaini makubaliano maalum, huku mfuko wa maendeleo ya kilimo ukitoa msaada kwa mpango wa uwekezaji kwenye kilimo.

Mpango huo unaangalia uongezaji wa thamani, miundombinu ya kilimo, masoko na biashara, mfumo wa taarifa za kilimo, usalama wa chakula, mazingira na maliasili pamoja na utawala bora na maendeleo ya taasisi.

Naye Mwezeshaji Abdul Chacha, akiwasilisha mada kuhusu uimarishaji ushiriki na uandishi wa habari za SADC katika viwanda, kilimo na biashara, alisema bado vyombo vya habari havijafanya kazi ya kuhakikisha taarifa zinawafikia wananchi wengi zaidi.

Alisema pato la taifa kwa nchi hizo limekuwa kutoka dola za Marekani 1,912 hadi 2,454, huku nchi inayoongoza ni Visiwa vya Seychelles ikiwa na asilimia 7.9 ikifuatiwa na Tanzania yenye asilimia 7.0.

Kwa mujibu wa Chacha, kwenye sekta ya uzalishaji Tanzania na Zimbabwe zilikuwa na ukuaji wa kati ya asilimia 12.1 hadi 9.3 mwaka 2018 huku DRC ikiporomoka kwa asilimia 0.8.

Kwa upande wa biashara, mwaka 2018 usafirishaji wa bidhaa ndani ya nchi wanachama ilikuwa ni Dola bilioni 154 na uagizaji kwenye nchi ni zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 149.

Katika kikao hicho vyambo vya habari vikiongozwa na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA-TAN), vilikubaliana kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali kuripoti habari za kina ili kuwaelimisha wananchi.



Wasamaria wema wakisaidia kusukuma gari ya abiria katika eneo la Mbande Chamazi baada ya kuzimika ghafla jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: RAMADHAN ISMAIL-TUDARCO**

# Samia aipongeza CRDB kwa kusaidia upasuaji moyo watoto

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuandaa mbio za hisani zilizokusanya zaidi ya Sh. milioni 200, ili kusaidia watoto wenye uhitaji wa upasuaji moyo Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Samia alisema CRDB inasaidia jitihada za serikali katika kutoa huduma bora za afya kwa watoto na kuongeza uelewa kwa jamii kuhusiana na magonjwa ya moyo kwa watoto.

"Kupata huduma bora za afya ni haki ya kila binadamu, haki ambayo ni muhimu katika maendeleo ya kila binadamu, hususan watoto wetu na vijana katika kukua vizuri na kuwa na afya njema," alisema.

Pia aliwapongeza washiriki na kampuni zilizoshiriki kuandaa mbio hizo maarufu 'CRDB Bank Marathon' kwa kuungana kwa pamoja kukusanya fedha kwa ajili ya kusaidia upasuaji wa watoto, huku akiwataka watu wote kuendeleza jitihada hizo.

"Upo usemi usemao ukiokoa maisha ya mtu umeiokoa dunia, jitihada hizi zisiishie hapa, tuendelee kushirikiana na taasisi yetu ya moyo katika kurejesha tabasamu kwa watoto wetu," alisisitiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema mbio hizo za hisani zilizoshirikisha watu 4,000 zimevuka lengo la kiwango kilichowekwa cha Sh. milioni 200.

Alisema mbio hizo zilizokuwa na kaulimbiu ya 'Kasi Isambazayo Tabasamu' zimewaunganisha washiriki kwa pamoja kuchangia fedha hizo zinazoelekezwa kwenye upasuaji wa moyo kwa watoto.

Kadhalika alisema kwa muda mrefu CRDB kupitia sera yake ya kusaidia jamii (CSR Policy), imesaidia Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kufanya upasuaji kwa watoto ili kuongeza ushiriki wa jamii kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii ikiwamo changamoto ya upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watoto na mbio hizo zitakuwa zikifanyika kila mwaka.

"Michezo ina nguvu ya kuwahamasisha watu kushiriki katika mabadiliko chanya. Ni furaha kubwa sana kwetu kuona mbio hizi za hisani za CRDB Bank Marathon zinachochea mabadiliko chanya katika jamii na kuongeza ushiriki wa watu katika kutatua changamoto na kuleta maendeleo. Naye Waziri wa Habari, Michezo, Vijana na Utamaduni, Dk. Harison Mwakyembe, alipongeza benki hiyo na wadau walioshiriki katika mbio hizo kwa mchango wao walioutoa kusaidia upasuaji wa moyo kwa watoto.

"Benki ya CRDB imeonyesha sio tu ni bora kwa kutoa huduma bora kwa wateja, lakini pia ipo mstari wa mbele kusaidia jamii kwa sababu uongozi wa benki hii unaelewa taifa lolote lenye mafanikio ni lazima kuwekeza katika afya ya watoto," alisema Dk. Mwakyembe.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Prof. Mohammed Janabi, alisema kwa sasa wapo watoto 500 katika orodha ya taasisi hiyo wanaosubiria kufanyiwa upasuaji wa moyo huku wazazi na walezi wao wakishindwa kumudu gharama za matibabu.

Aliishukuru benki hiyo kwa kuandaa mbio hizo na kuwaomba wadau wengine pia kujitokeza kusaidia.

"Nimeshiriki mbio nyingi, lakini mbio hizi za hisani zilizoandaliwa na Benki ya CRDB ni za kipekee sana kwa sababu tunapata nafasi ya kusambaza tabasamu kwa washiriki wenzangu na kwa watoto," alisema Boniface Ngwata mshindi wa mbio za baiskeli kilomita 42.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, klabu wadhamini zaidi wanahitajika kuiboresha ligi

**TUMESHUHUDIA** msimu wa Ligi Kuu Bara 2019/20 ukimalizika kwa changamoto nyingi, ambazo ziliufanya kuwa mgumu zaidi kuwahi kutokea katika historia ya ligi yetu na pengine duniani kote, hata hivyo kwa Tanzania Bara ukimalizika kwa Klabu ya Simba kutwaa ubingwa huo pamoja na Kombe la FA.

Tunasema msimu uliomalizika wa 2019/20 ulikuwa mgumu kuwahi kutokea hasa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, ambao ulisababisha Ligi Kuu Bara kusimama kwa muda wa miezi mitatu huku ligi zingine duniani zikilazimika kufutwa na zingine ziliporejea zikachezwa bila mashabiki, lakini pia zikichelewa kumalizika kama ilivyokuwa hapa nchini.

Mbali na changamoto hiyo, pia kwa Ligi Kuu Bara tumeshuhudia ugumu wa ligi hiyo husussan timu zilizokuwa zikihaha kujinusuru kushuka daraja, vita ambavyo vilienda hadi mechi za mwisho za msimu huu ambao timu tano zilishuka huku tatu kutoka Ligi Daraja la Kwanza zikipanda.

Singida United ilikuwa ya kwanza kupoteza tiketi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao ikifuatiwa na Ndanda FC, Alliance FC, Lipuli FC huku Mbeya City ikiponea kwenye mechi za mchujo kwa kuitoa Geita FC ya Daraja la Kwanza, lakini Mbao FC nayo ikikwaa kisisi kwa Ihefu FC hivyo kushuka.

Ni dhahiri, kushindwa kufanya vizuri kwa timu nyingi ikiwamo kwenye mbio za ubingwa zilizoongozwa kwa asilimia kubwa na Simba hadi mwisho kabla ya kuutwaa na zile zilizoshuka, kulisababishwa na uchumi mbovu ulioziandama huku baadhi zikishindwa kulipa wachezaji mishahara kwa wakati na kusafiri kwa tabu kutoka kituo kimoja hadi kingine wakati wa mechi.

Mafanikio ya Simba ya kutwaa mataji matatu msimu huu; Ngao ya Jamii, Ligi Kuu na Kombe la FA, yametokana na kutotikisika kiuchumi kwa wachezaji wao na benchi la ufundi kulipwa kwa wakati, kula vizuri, kambi nzuri na hata kusafiri kwa ndege kwa safari ndefu jambo ambalo lilikuwa vigumu kwa timu nyingi. Ukiacha Simba, Azam FC, Yanga ambayo nayo imepitia vipindi vigumu kiuchumi msimu uliomalizika, timu nyingine zenye unafuu kiuchumi ambazo hazikuwa na mtikisiko wa kulipana mishahara na usafiri ni KMC, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar, Ruvu Shooting, JKT Tanzania na Polisi Tanzania pengine na Alliance ilishuka daraja.

Kwa sasa tayari Bodi ya Ligi nchini (TPLB), imetangaza ligi hiyo itaanza rasmi Septemba 6, mwaka huu huku klabu zikiwa katika hekaheka za kuimarisha vikosi vyao baada ya dirisha la usajili kufunguliwa Agosti Mosi, mwaka huu na likitarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu. Kwa maandalizi yanayofanywa kwa upande wa usajili, ni matarajio yetu Ligi Kuu itakuwa ngumu zaidi msimu ujao.

Hivyo, kitengo cha masoko cha Shirikisho la Soka nchini, hakina budi kuzama sokoni kushawishi wadhamini zaidi kujitokeza kuidhamini ligi hiyo, jambo litakalozifanya klabu kupata mgao mkubwa wa haki za matangazo na kuzisaidia kuimarika kiuchumi na ushindani kuongezeka hivyo ligi kuwa bora zaidi.

Lakini hatuna budi kuzikumbusha klabu kutotegemea sana mgao wa wadhamini kutoka TFF pekee, kwani jukumu la kujiimarisha kiuchumi ni la klabu na si la shirikisho hilo, hivyo wakati huu zikiendelea na maandalizi kuelekea msimu mpya, ni wakati kwao kutafuta wadhamini wengi iwezekanavyo.

Ikumbukwe mdhaminni mkuu wa ligi hapaswi kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa klabu, kwani hilo ni jukumu kwa kila klabu kujitafutia wadhamini wake mfano wa jezi na vifaa vingine vya michezo ili kujiimarisha kiuchumi na kuacha kutegemea mapato ya mlangoni ambayo kwa kiasi kikubwa kwa sasa yamepungua kutokana na mechi kurushwa mubashara kupitia Azam TV.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Yanga sasa iachane na Morrison, isonge mbele

**WIKI** iliyopita kulitokea tukio ambalo liliwakusanya mashabiki wengi wa soka kwenye Ofisi za Shirikisho la Soka nchini (TFF), baada ya mchezaji Benard Morrison kuishtaki Yanga kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kuhusu mkataba wake na klabu hiyo.

Kamati hiyo ilichukua siku tatu kabla ya kutoa maamuzi kuwa mkataba wa Yanga na mchezaji huyo una mapungufu, hivyo ikamuachia mchezaji huyo huru kujiunga na klabu yoyote ile ndani na nje ya nchi.

Wakati huo huo, tayari Agosti 8, Morrison alikuwa amesaini kwenye klabu ya Simba na kutambulishwa rasmi.

Baada ya maamuzi hayo ambayo waliteka hisia za wanamichezo wengi nchini, ambao siku tatu nzima walikuwa wamekusanyika kwenye ofisi hizo na wengine kufuatilia kwenye vyombo vya habari na hata mitandao ya kijamii, hatimaye Morrison alishinda shauri lake. Uongozi wa Yanga ulitoa taarifa kuwa hauridhiki na maamuzi hayo, hivyo ulitoa taarifa kuwa utakata rufani kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Masuala ya Michezo (GAS).

Mwenyekiti wa Kamati hiyo iliyohukumu suala hilo, Elius Mwanjala akaibuka na kuitaka Yanga kutokwenda kwanza CAS, badala yake ikate rufani na kulirudisha tena suala hilo kwenye kamati hiyo hiyo ili lipitiwe upya.

Kwenye kikao chao, viongozi wa Yanga walimjibu kuwa hawatofanya hivyo tena, badala yake watakwenda moja kwa moja CAS.

Kwanza napenda niwapongeze viongozi wa Yanga kwa kuamua kutolirudisha tena suala hilo kwa ajili ya kupitiwa upya kwa sababu nyingi tu, ikiwamo hata suala la muda. Kingine ninachowashauri viongozi wa Yanga ni kwamba waachane hata na suala la kwenda CAS, kwani kama ilivyo iwapo wangelirudisha tena TFF, litawapotezea muda na gharama nyingi ambazo zingeweza kufanyiwa vitu vingine vya maendeleo.

Gharama ambazo watatumia kupeleka suala lao huko, zinaweza hata kusajili wachezaji wengine wazuri zaidi ya Morrison.

Lakini pia hata suala hilo likipelekwa huko, halitoamuliwa leo wala kesho, lakini halitomzuia Morrison kuichezea klabu anayoitaka. Ni kwamba hatozuiwa kuichezea Simba. Ataendelea kucheza huku suala likisikilizwa.

Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) kwa sasa halimfungii mchezaji yeyote mwenye matatizo ya mkataba, badala yake linampa kibali cha muda cha kucheza soka huku suala lake likiendelea kusikilizwa, hivyo bado Yanga itakuwa haijatibu tatizo, au kutaka inachokitaka.

Vile vile, Morrison anaonekana kabisa hana nia ya kuichezea klabu hiyo, hivyo hata kama ikishinda shauri pia itaonekana kama ni kazi bure tu, huku muda na pesa vikiwa vimepotea.

Ni kwamba viongozi wa Yanga kipindi hiki cha usajili wasiyumbishwe na mchezaji mmoja, badala yake waachane naye na waangalie wachezaji wengine wazuri zaidi, kwani wakijichanganya kipindi hiki cha usajili, baadaye watawekwa kikaangoni na wanachama na mashabiki ambao watawauliza ni kwa nini timu haikusajiliwa vizuri. Kumbe wakati huo viongozi walikuwa bize na suala la Morrison.

Klabu ya Yanga imeshakuwa na wachezaji wengi wazuri, mahiri na wenye vipaji vya hali ya juu kuliko Morrison, lakini kwa sasa hawapo, kwa kustaafu au walihama, na klabu imeendelea kuwapo, tena kubwa na maarufu, ikiwa na wanachama wengi sana nchini na Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kinachotakiwa kwa sasa viongozi wa Yanga ni kutulia na pesa zilizopangwa kwenda CAS, zikasajili mchezaji au wachezaji mbadala ambao watakuwa na moyo wa kuichezea klabu hiyo kwa mapenzi na si kwa kulazimishwa.

Kosa kubwa ambalo viongozi wa Yanga watafanya ni kuendelea kung'ang'ana na suala hilo la Morrison ambalo haliwezi kuwasaidia kitu, kwani hata akipatikana wao wenyewe hawatomwamini tena na mchezaji mwenyewe mapenzi yake hayatoweza tena kuwa kwenye klabu hiyo, zaidi watamkomoa kama ambavyo wanadaiwa kutaka kufanya.

Inawezekana kabisa hii ikawa ni mbinu ya kuwatoa kwenye mawazo ya kutafuta wachezaji bora kipindi hiki, halafu baadaye timu iwe dhaifu na isiweze kupigania tena ubingwa kwa mara nyingine.

Viongozi wa Yanga waamke na kujikita zaidi kwenye usajili wa wachezaji bora wenye moyo wa kuitumikia timu, waachane na suala la Morrison ambalo litawapotezea muda na pesa pia, kwa mchezaji ambaye ameonekana hana mapenzi na klabu yao, badala yake iendane na kaulimbiu yao ya "Yanga Daima Mbele Nyuma mwiko."

# Madereva malori walalamikia waajiri

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

MADEREVA wa magari makubwa yanayosafirisha mizigo ndani na nje ya nchi wamelalamikia kitendo cha baadhi ya wamiliki wa magari hayo kushindwa kuajiri madereva wawili kama sheria inavyotaka huku wakilazimishwa kusafiri nje ya nchi zaidi ya mara tatu kwa mwezi hali inayotajwa kuchangia ajali.

Wakizungumza katika kikao cha pamoja baina na madereva hao na Jeshi la Polisi mkoa wa Morogoro, walisema ajali nyingi zinazotokea huchangiwa na uchovu wa kusafiri umbali mrefu bila kupumzika. Juma Msakale mmoja ya madereva hao, alisema hali hiyo inachangiwa na baadhi ya waajiri kuwalazimisha kusafiri nje ya nchi zaidi mara tatu hadi nne bila kuajiri madereva wawili kama inavyotakiwa. "Vyanzo vya ajali ni hizi kampuni zinampangia dereva kwenda Congo kwa mwezi mara tatu, na akienda chini ya hapo anakatwa mshahara au gharama ziwe zake kwa hiyo dereva hapumziki ili awahi muda aliopangiwa ndio maana tunachoka unakuta mtu anasababisha ajali," alilalamika Msakale.

Naye Jacob Amos, aliyewahi kupata ajali kutokana na uchovu wa barabarani, alisimulia kuwa hali hiyo ilimkuta wakati akijaribu kuwahisha mzigo ndani ya muda aliopangiwa na mwajiri wake ili kuepuka adhabu ya kukatwa mshahara. Alisema suala hilo linawawia vigumu kupingana nalo kwa sababu ya ugumu wa maisha licha ya kwamba wanajitahidi kuwa na tahadhari barabarani na kuliomba Jeshi la Polisi na serikali kusimamia ipasavyo sheria ya uwapo wa madereva wawili.

"Binafsi niliwahi kupata ajali baada ya kusinzia barabarani wakati naendesha gari kwasababu niliendesha umbali mrefu bila kupumzika, lakini kama serikali itatilia mkazo suala la kuajiri madereva wawili kwa sisi ambao tunasafiri hadi nje ya nchi itasaidia kuondokana na ajali hizo," alisema Jacob.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, aliwatahadharisha wamiliki wa malori kuzingatia sheria za nchi na kuwapa muda wa kupumzika madereva wao.

Alisema kuwa ni vyema kila mmiliki kwa nafasi yake kukatii sheria bila shuruti ili kulinda maisha ya watu na mali wanazomiliki badala ya kusubiri vyombo vya dola kuanza kutumia nguvu katika kusimamia sheria zilizowekwa.

Aliwataka madereva kujipa muda wa kupumzika ili waweze kuvitambua na kuviepuka vyanzo vya ajali pamoja na kuheshimu sheria za barabarani na kuongeza umakini wanapoendesha vyombo vyao barabarani.




Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga (katikati), akikata utepe kuzindua duka la kisasa la Vodacom mjini Lindi mwishoni mwa wiki, kuwafikishia wananchi huduma karibu. Kushoto ni Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Pwani na Dar es Salaam, Brigita Stephen na Meneja wa Vodacom Lindi, Omary Kilumanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Migogoro ya vijiji, hifadhi kutatuliwa

**Na Beatrice Shayo**

TUME ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imesema inaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vyote vinavyoizunguka hifadhi nchini, ili kuondoa migogoro iliyodumu kwa miaka mingi kati ya wananchi na hifadhi za wanyamapori.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Nindi Stephen, wakati akitoa mada kwa njia ya mtandao kwa Chama cha Waaandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) yaliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Alisema Tume kwa kushirikana na Wizara ya Maliasiali na Utalii, kwa kutambua umuhimu wa bainowai, wameanzisha mpango huo, lengo kubwa likiwa kuondoa migogoro kati ya wananchi na hifadhi za wanyamapori.

"Lengo ni kuwahifadhi wanyama kwa ubora zaidi pamoja na kupunguza chokochoko ambazo wananchi wamekuwa wakiingia kwenye hifadhi za taifa na kusababisha manung'uniko kila wakati," alisema.

Alisema mpango huo umeshaanza kwa kiasi kikubwa katika katika hifadhi za Taifa za Serengeti, Manyara na Tarangire, na timu yake imeshamaliza kazi katika maeneo hayo na wataendelea kwenye hifadhi zilizobaki.

Alisema wanashirikiana na kijiji kutafuta mifubo bora ya kuhifadhi wanyamapori kupitia mipango bora ya matumizi ya ardhi kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Wakala wa Misitu nchini (TFS).

Dk. Stephen alisema tume hiyo ni chombo cha kitaifa ambacho kazi yake kubwa ni kusaidiana na sekta binafsi katika kuhakikisha wanaandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha mipango hiyo inasaidia katika ulinzi wa bainowai.

Aidha, alisema tume hiyo kazi yake kubwa ni kuandaa mpango bora wa matumizi ya ardhi ambao tayari ulishaanza tangu mwaka 2013, na kuwa utadumu kwa miaka 20 hadi mwaka 2033.

# Mbunge wa zamani aonya kuwapitisha wala rushwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

VYAMA vya siasa vimeshauriwa kuepuka kuwapitisha wagombea watoa rushwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ili kuepusha taifa na viongozi wasiofaa.

Ushauri huo umetolewa na mbunge wa zamani wa Jimbo la Kigamboni, Frank Magoba (CUF), wakati akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa.

Alisema wakati wa mchakato wa kura za maoni wameshuhudia baadhi ya watia nia wakitoa rushwa kwa wajumbe ili wapate upendeleo wa kupitishwa na kuwa wagombea, jambo ambalo viongozi wengi walipigia kelele kuepusha kupata viongozi wasiofaa. "Ni wajibu wa wanasiasa kuelewa kuwa kukubali kuwapitisha wagombea watoa rushwa ni kuendelea kulipeleka taifa shimoni, na ikifikia hatua hiyo taifa linaweza kutumbukia kwenye machafuko ya wanaokosa haki kudai kwa nguvu," alisema.

Magoba alisema Rais Dk. John Magufuli ni kiongozi wa mfano ambaye anachukia watu wanaosaka uongozi kwa rushwa hivyo ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vingine vya siasa wasimwangushe katika mapambano dhidi ya vita hiyo. "Rais Magufuli amekuwa mstari wa mbele kuyaibua madudu yanayofanywa na watendaji wake hata pale madudu hayo yanapofichwa yeye huwa anayaibua na kutoa maamuzi pale pale, huo ndio uongozi wa Watanzania walio wengi walikuwa wanautaka," alisema.

Magoba aliwapongeza viongozi wa upinzani ambao wamekua mstari wa mbele kuikosoa serikali kwa nia ya kuifanya iwajibike ipasavyo katika kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Alisema wakati wa vikao vya Bunge, baadhi ya wabunge wa upinzani walisimama kidete na kusimamia hoja zao ambazo nyingi zilikuna na mashiko, japo mapokeo ya wabunge wa chama tawala yalikuwa tofauti.

Aliongeza kuwa pamoja na kazi zote zilizofanya na wapinzani baadhi ya Watanzania mtazamo wao ni kudhani yanayotekelezwa na serikali hakuna mchango wao.

# Wakulima wafurahia kuagiziwa mbolea

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAKULIMA wa mazao ya chakula ambao ni wanachama wa vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa mkoani hapa wamesema wamefurahishwa na mpango wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima cha Iringa Farmers Co-operative ( IFCU 1993) kwa kuanza kuwaagizia mbolea kutoka nje.

Wakizungumza wakati wa hafla fupi ya ufunguzi wa uuzaji wa mbolea iliyofanyika juzi katika kijiji cha Isalavanu, wakulima hao walisema hatua hiyo itawasaidia kukuza uzalishaji wa mazao yao na kujiongezea kipato zaidi.

Obadia Sanga na Sarah Kalinga, walisema kabla ya kuanzishwa kwa mpango huo walikuwa wakilazimika kununua pembejeo za kilimo hasa mbolea kwa gharama kubwa zaidi mjini Mafinga au Iringa, lakini kupitia mpango wa chama hicho, wanasogezewa mbolea hadi kijijini kwa gharama ya chini zaidi. Mwenyekiti wa IFCU 1993, Victor Mwipopo, alisema chama hicho kimeanzisha utaratibu huo ili kumkomboa mkulima na kuwa kutokana na mbolea hizo kuwa ni mkopo ambao unatakiwa kulipwa ndani ya miezi mitatu hadi ifikiapo Septemba 30, itawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji.

Alisema kuwa utaratibu utakaotumika kusambaza mbolea hizo ni kuuza kwa pesa taslimu kwa mkulima yeyote mwenye uwezo wa kununua mbolea hizo, lakini kipaumbele cha kwanza ni mkulima mwanachama wa ushirika na bei za mbolea hizo zimepangiwa bei elekezi na TFRA ya Sh. 50,000 kwa DAP na Sh. 43,500 kwa UREA kwa mfuko wa kilogramu 50 na wakulima wasio wanachama mbolea hiyo itauzwa kwa Sh. 53,000 kwa DAP na Sh. 45,000 kwa mfuko wa UREA wa kilogramu 50. Kuhusu mafanikio ya chama alisema, chama hicho kimeagiza na kununua mbolea tani 274 kupitia mfumo wa ununuzi wa pamoja (BPS), kuanzisha mradi wa 'Farm Clinic' katika kijiji cha Ihemi kilichopo Iringa Vijijini kwa kununua shamba lenye ukubwa wa ekari nne.

Alisema chama kimenunua eneo lililopo kijiji cha Vitono kwa ajili ya kujenga ghala ambalo litasaidia wanachama kuhifadhi mazao na kuuza kwa pamoja, kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi mazao ghalani.

Pia chama kimenunua zana za kilimo ikiwamo mashine ya kubota kwa ajili ya kuvisaidia vyama wanachama vinavyolima mazao mbalimbali, ili wanachama waweze kulima kwa wakati na kwa bei rafiki na kwa sasa mashine hiyo ipo Chama cha Msingi Igomaa Umwagiliaji (CHUI) na kufufua vyama vilivyokuwa sinzia kwa muda mrefu.

# Bandari Dar yaanza kupokea meli toka Ulaya, Asia

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amesema Bandari ya Dar es Salaam imeanza kupokea meli kubwa kutoka nchi za Ulaya na Asia ambazo zilikuwa hazifiki kutokana na miundombinu ya awali.

Akizungumza wakati wa ziara ya ukaguzi maboresho yanayoendelea katika bandari hiyo, Kamwelwe alisema meli nyingi hususani kubwa zilizokuwa zikitoka katika mataifa hayo zilitumia Bandari ya Mombasa nchini Kenya kupitishia mizigo ya Tanzania.

"Meli nyingi kubwa zilizokuwa zinakwenda Mombasa nchini Kenya halafu mizigo inapakuliwa na kuwekwa kwenye meli ndogo, ndipo zinaletwa kwetu na hiyo ilikuwa inaongeza gharama kubwa, lakini sasa zinakuja moja kwa moja kutoka Ulaya na Asia mpaka Bandari ya Dar es Salaam bila kufanya 'transfer' kupita kwenye bandari za nchi nyingine," alisema Kamwelwe.

Waziri huyo alisema meli hizo kwa sasa zinaingia bandarini humo baada ya upanuzi na matengenezo makubwa, na kinachofanyika kwa sasa ni utekelezaji wa mradi wa kuongeza kina cha maji cha mita 13 kwa kuhamisha sehemu ya bahari na kuwezesha meli kubwa za aina yoyote kutoka duniani kutia nanga.

Kamwelwe alisema lengo ni kuteka soko lote la Afrika Mashariki na nchi zilizopo katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kuhakikisha mizigo yote inayokwenda katika nchi hizo inapitia katika bandari za Tanzania.

Pia alisema matengenezo yanayoendelea ni upanuzi, uimarishaji na uboreshaji wa bandari katika maeneo ya magati, yadi zenye uwezo wa kupokea magari 3,000 kutoka 170,000 kwa wakati mmoja, na lengo ni kufikia magari 200,000 pamoja na kuongeza kina cha maji. "Pamoja na meli hizi kubwa kuingia nchini, lakini tulijipanga zitumie muda mfupi kupakua mzigo, ambao ni kiwango cha kimataifa.

"Lakini uwezo wetu ni mkubwa kwa sababu gati la kupakia meli za magari tumeongeza kwenye kina chenye mita 13 cha sehemu ya maji ya bahari pamoja na sehemu ya lango la meli zinakoingilia za mita 10.5. Pia tayari tumeshafanya manunuzi tunasubiri Benki ya Dunia (WB) ili tuingie mkataba wa kuongeza sehemu nyingine ya kina cha maji kwenda mita 17," alifafanua Kamwelwe.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Deusdedit Kakonko, alisema idadi ya meli zinazotia nanga katika bandari hiyo ni 250 kwa mwezi kutoka 180 za mwishoni mwa mwaka jana, na kwamba wamejipanga kuvutia wateja zaidi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo (kulia), akimwonyesha Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatama (aliyekaa), namna kiwanda hicho cha kuchakata samaki kitakavyokuwa baada ya kukamilika kwa ukarabati unaoendelea, alipokitembelea mkoani Rukwa mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi, Stephen Lukanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri alishtukia dampo hatari

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Sima, ameghadhabishwa na ujenzi duni wa dampo la taka la Nsalaga Uyole, mkoani Mbeya, na kuonya kwamba miundombinu hiyo ni hatari kwa afya za watu na mazingira kwa ujumla.

Amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC) kushirikiana na ofisi za Mkoa wa Mbeya ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo, kwani dampo limejengwa bila kuzingatia kanuni za kuhifadhi mazingira na pia utupaji taka kwenye dampo umekuwa ukirudisha uchafu kwenye makazi ya watu.

Kwa mujibu wa Sima, taarifa alizopata dampo limejengwa bila utafiti wa kitaalamu wa kutosha.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo la Nsalaga Uyole, katika ziara yake ya kikazi kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, alisisitiza kwamba taka lazima zitenganishwe kwenye vyanzo kabla ya kuingizwa kwenye dampo.

"Kuanzia sasa watafutaji taka wasiruhusiwe kuingia kwenye mashimo ya dampo kwani wamekuwa wakirudisha uchafu kwenye makazi ya watu na kuchafua mazingira," alisema.

Sima ambaye aliambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Prof. Esnati Chaggu, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka na maofisa wengine wa baraza hilo, aliwataka wasimamizi wa dampo hilo kujifunza kutoka kwa wasimamizi wa madampo katika mikoa mingine ambako madampo ya kisasa tayari yamejengwa na yanahifadhi mazingira.

"Halmashauri ya Mkoa wa Mbeya mjipange na kuhakikisha mnatenga eneo maalum ya shughuli za urejelezaji ili kuondoa mrundikano wa uchafu, kwani mmekuwa mkichanganya uchafu na taka ngumu ambazo ni ngumu kuzizoa," aliagiza naibu waziri huyo.

Prof. Chaggu alisema majitaka yatokayo katika dampo yana sumu kiasi kikubwa na kufafanua kwamba majitaka hayo yana asilimia nane juu ya majitaka yatokayo majumbani.

Alishauri majitaka hayo yasimamiwe kwa umakini ili yasititirike katika mazingira na kudhuru jamii inayoishi karibu na dampo hasa katika kipindi cha mvua.

Dk. Gwamaka kwa upande wake alifafanua kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni za Usimamizi wa Taka ngumu, halmashauri za wilaya zina wajibu wa kutenganisha taka na kuelimisha wananchi jinsi ya kufanya hivyo.

Alifafanua kuwa taka ni fursa na kutoa mifano kwamba taka za glasi na plastiki zinaweza kuwa malighafi kwenye viwanda vya urejelezaji na kukuza uchumi kwani viwanda vinalipa kodi kwa serikali.

HABARI KITAIFA

# Ummy afurahishwa kasi ujenzi hospitali ya rufani

**Na Renatha Msungu,** GEITA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amefurahishwa na kasi ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita unaotekelezwa na Wakala wa Majengo nchini (TBA).

Katika ziara yake Waziri Mwalimu akiwa katika eneo la mradi alieleza kufurahishwa na kasi ya ujenzi huo na kuipongeza TBA kwa kuendelea kutekeleza mradi huo katika ubora.

"Nawapongeza TBA kwa kazi nzuri wanayoifanya, hili jengo ni zuri na linastaili kuwapo hapa," alisema.

Aidha, Waziri Ummy aliishukuru serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na mingine ya afya kote nchini.

Vile vile, aliipongeza TBA kwa kuendelea kutekeleza miradi katika kiwango cha juu, huku akiitaka kuendelea kujenga majengo bora sehemu nyingine.

Aidha, alimpongeza Meneja wa TBA Mkoa wa Geita, Mhandisi Gladys Jefta, kwa kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha ujenzi unakwenda vizuri.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, aliipongeza TBA kwa kazi nzuri iliyofanyika katika ujenzi wa hospitali hiyo.

Akiishukuru serikali kwa kuleta mradi huo na kwamba utasaidia kuokoa maisha ya wanawake wengi wakati wa kujifungua pamoja na wagonjwa wengine watakaopata huduma katika hospitali hiyo ya rufani.

Jefta alimshukuru Waziri Ummy kwa kutembelea mradi wa afya ambao unatekelezwa na TBA kwa mfumo wa buni - jenga.

Aklisema amefarijika sana kuona waziri ametambua kazi inayofanywa na TBA kuwa ni yenye ubora na ameahidi kuyafanyia kazi yale yote ambayo waziri aliyaagiza.



Naibu wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, akizungumza kwenye hafla ya mtandao wa wafanyabiashara wakubwa na wakati ambao ni wateja wa NMB Kanda ya Ziwa, iliyofanyika jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W/biashara wasisitizwa kujiunga mtandao NMB

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAFANYABIASHARA nchini wamehimizwa kujiunga na Mtandao wa Wafanyabiashara wateja wa benki ya NMB (NBEN) ili kujua na kunufaika na fursa za elimu juu ya mpangilio na uendeshaji biashara, kodi na taratibu za serikali kuhusu biashara.

Akizungumza jijini hapa juzi wakati wa mkutano wa mtandao wa wafanyabiashara wateja wakubwa wa NMB Kanda ya Ziwa, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Filbert Mponzi, alisema wafanyabiashara wanaojiunga na mtandao huo pia hupata fursa kukutana na kujadiliana ana kwa ana na uongozi wa juu wa benki hiyo.

"Kupitia vikao vya kila mwaka vya NMB Business Executive Network inayohusisha wafanyabiashara wa kati na wakubwa, wafanyabiashara hupata elimu kutoka kwa wataalamu wa fani mbalimbali kuhusu namna bora ya kufanya biashara kirahisi, kwa tija na gharama nafuu kupitia teknolojia," alisema Mponzi.

Mtandao huo ulioanza mwaka 2014, tayari unajumuisha wafanyabiashara zaidi ya 300 kutoka miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Kilimanjaro, Mtwara na Morogoro.

"Hata wafanyabiashara wasiyo wateja wa NMB wanaweza kujiunga na mtandao wa NBEN kuona fursa, bidhaa na huduma zinazotolewa na benki yetu inayoongoza kwa faida baada ya kodi na ubora kwa miaka 11 mfululizo," alisema Mponzi.

Mkuu wa kitengo cha biashara wa NMB, Alex Mgeni, aliwataka wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla kutumia huduma ya bima inayotolewa na benki hiyo ili kupata fidia kwa haraka na wakati kupitia matawi zaidi ya 220 nchini.

"Tayari tumezindua huduma ya bima za aina mbalimbali ikiwamo ya mazao ya kilimo itakayowawezesha wakulima kupata fidia ya madhara na uharibifu unaotokana na majanga kama mafuriko, ukame, uharibifu wa wadudu na ndege waharibifu," alisema Mgeni.

Naibu wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula aliyekuwa mgeni rasmi katika mkutano huo, aliipongeza benki hiyo kwa kuanzisha bima ya mazao ya kilimo na kuutaka uongozi kuongeza kasi ya elimu kwa umma kuhusu bidhaa na huduma hiyo.

"Bima ya mazao itanufaisha na kuongeza tija katika sekta ya kilimo ambayo mnyororo wake wa thamani unahisisha zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. Endeleeni kuelimisha umma kuhusu huduma na bidhaa," alisema Mabula.

# Watumishi wapewa jukumu kuupaisha mkoa

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amewaagiza watendaji wa sekta mbalimbali kuhakikisha wanafanyakazi kwa bidii ili mkoa huo uwe unashika nafasi za juu kitaifa.

Alitoa agizo hilo wakati wa mkutano na wananchi katika Viwanja vya TASAF wilayani Sikonge wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo kwenye maeneo mbalimbali.

Dk. Sengati alisema haiwezekani mkoa huo wenye historia kubwa katika harakati za kudai Uhuru ukashika nafasi chini ya kumi bora katika elimu, afya, kilimo, ufugaji bora na sekta nyingine.

Alisema ni lazima wasimamizi na watumishi wa sekta zote wafanyekazi kwa kujituma na uadilifu kwa ajili ya mkoa kufanya vizuri na kushika nafasi ya kwanza ili uwe darasa la mikoa mingine kuja kujifunza jinsi walivyofanikiwa.

Aliongeza kuwa msimamizi wa sekta ambayo itafanya vibaya na kuupelekea mkoa kushika nafasi za chini ya 10 bora atachukuliwa hatua ikiwamo kuondolewa katika nafasi yake.

Alisema anapenda mtumishi ambaye anajituma kwa kufanyakazi kwa weledi, ubunifu na anayependa kuwatumikia wanyonge kwa ajili ya kuwaletea maendeleo na mafaniko.

"Mimi nampenda mtumishi ambaye ni mchapakazi…anasaidia kubuni miradi inayowaletea maendeleo na asiyependa rushwa kama mimi na anayenda kutumia wananchi kwa misingi ya haki…lakini mimi ni adui ya mtumishi anayenda rushwa na asiyekuwa mbunifu," alisisitiza.

# Shirika laongeza thamani ya mazao

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SHIRIKA la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) limesema limeweza kuongeza thamani ya mazao ya mboga na viungo kupitia vikundi mbalimbali vya wakulima wanaojihusisha na kilimo hai kitendo kilichokuza uchumi wa wakulima hao.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa shirika hilo, Janet Maro, ambapo wakulima wapatao 10,250 kutoka mikoa ya Morogoro na Dodoma kupitia vikundi vyao wamenufaika na kilimo hai kutokana na mazao yao kuuzwa nje ya nchi.

"Shirika hili linalojihusisha na kilimo hai kisichotumia dawa za kemikali limekuwa likinunua mazao ya wakulima wanaolima kilimo hai na kuyachakata kicha kuyasafirisha nje ya nchi mbalimbali zinazoyahitaji," alisema Janet.

Alisema shirika limekuwa likiwahamasisha wakulima kupitia vikundi vyao kulima mazao kwa kutumia kilimo hai ambacho kina tija kutokana na mazao hayo kuwa na soko kubwa nchi za Ulaya kitendo lilichoongeza sana thamani yake. Janet alisema kuwa kutokana na uhitaji wa mazao ya mboga na viungo kama vile karafuu waliamua kuunda vikundi vya wakulima na kuwapa mkataba kwa ajili ya kuzalisha mazao hayo ambapo nao walihamasika kulima mazao hao kwa wingi.

Mwenyekiti msaidizi wa kamati ya wakulima ya uzalishaji masoko, kilimo cha matunda na mboga wilayani Mvomero, Mese Meena, alisema vikundi vya wakulima wanaozalisha mazao hayo SAT imewanufaisha kiuchumi.

Naye Mkurugenzi mstaafu wa shirika hilo, ambaye ni raia ya Ujerumani, Bernward Geier, aliipongeza SAT na kwamba alikuja nchini kuangalia namna inayofanya kazi inavyosaidia kuboresha maisha na wananchi.

# Mnada wauza mbaazi kilo 420,756

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JUMLA ya kilo 420,756 za mbaazi zimeuzwa na wakulima wa Wilaya ya Tunduru mkoani kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika mnada wa kwanza uliofanyika katika msimu wa mwaka 2019/2020 .

Katika mnada huo wa kwanza tangu zao hilo kuasisiwa na wakulima wa Tunduru ulifanyika katika viwanja vya ofisi za Chama cha Ushirika cha Mlingoti Maghalibi AMCOS, jumla ya wanunuzi kutoka kampuni mbili walijitokeza na kutoa bei tofauti, mnunuzi mmoja kati yao alishinda na kununua mbaazi hizo kwa bei ya shilingi 580 kwa kila kilo moja.

Kwa kutumia bei hiyo, jumla ya shilingi 244,038,480 zimepatikana na zinatarajiwa kusambazwa kwa wakulima waliokubali kukusanya katika AMCOS zao na kuuza mbaazi zao kupitia mfumo huo na kuongeza mzunguko wa fedha katika wilaya.

Alisema fedha hizo zitasambazwa kwa wakulima baada ya mshindi wa mnada huo kuingiza fedha kwenye akaunti ya chama kikuu na kukamilika kwa taratibu za makato ya kisheria ambayo ni wastani wa kati ya shilingi 84 hadi 99 kwa kilo moja iliyouzwa kupitia mfumo huo.

Bisani aliendelea kubainisha kuwa baada ya mauzo hayo, mkulima hukatwa kiasi hicho kutokana na gharama za chama Kikuu (TAMCU) shilingi 15, AMCOS shilingi 35 mchango wa Eeimu shilingi 2 na gharama za usafirishaji wa mazao ya mkulima kutoka AMCOS hadi ghala kuu la kuuzia mazao ni kati ya shilingi 47 hadi 70 kwa kila kilo moja ya mazao ya mkulima.

Alisema baada ya makato hayo wakulima ambao mazao yao yanasafirishwa kutoka umbali mrefu atalipwa kiasi cha shilingi 481 na wakulima ambao mazao yao yatasafiri umbali mdogo watalipwa kiasi cha shilingi 496 kwa kila kilo moja waliyouza kupitia mfumo huo.

Awali Kaimu Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, Goerge Bisani, alisema fedha hizo zinatarajiwa kulipwa kupitia utaratibu wa kuwalipa wakulima waliokubali kuuza mbaazi zao kupitia mfumo huo baada ya wanunuzi hao kuingiza fedha katika vyama vya ushirika vya wakulima vilivyo kusanya mbaazi zao na kuwaingizia fedha zao kwenye akaunti zao za mbenki.

Akizungumza kwa niaba ya Meneja wa TAMCU, Imani Kalembo, Yasini Masiano aliwataka wakulima walioshirki katika mnada huo kuwa makini kusikiliza bei zinazosomwa kutoka kwenye barua za wanunuzi walioomba kununua mazao yao ili waweze kuchagua bei kubwa kuliko zote.

Makamu Mwenyekiti TAMCU, Mussa Manjaule, aliwapongeza wanunuzi walioshinda na kununua mbaazi hizo kwa wakulima kwa wakati tofauti na awali.

# Shule yaomba mabweni ya wenye ulemavu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

UONGOZI wa Shule ya Msingi Kagondo B iliyoko wilayani Muleba mkoani Kagera ambayo ina wanafunzi wenye ulemavu, umeomba kujengewa mabweni kwa ajili ya wanafunzi hao.

Wanafunzi hao wakiwamo wenye ulemavu wa viungo, mtindio wa ubongo na viziwi kwa sasa wanalazimika kutumia bweni moja la Kolping ambalo liko mbali na shule, lakini limechakaa na halifai kwa matumizi.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada wa vyumba viwili vya madarasa vilivyojengwa na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Esta Rwamtoga, alisema shule hiyo yenye kitengo maalum, ina watoto wenye ulemavu mbalimbali wapatao 79 wakiwamo wa kike 38 na wa kiume 41. Mwalimu Rwamtoga alisema mbali na wanafunzi wenye mahitaji maalumu kukosa bweni pia wanalazimika kutumia chumba kimoja cha darasa, hivyo kuiomba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuwajegea vyumba vitatu vya madarasa kwa ajili ya watoto hao.

"Hapa kuna walemavu wa viungo, wapo wenye mtindio wa ubongo, pia wapo viziwi na wenye uoni hafifu kuwaweka katika chumba kimoja cha darasa wote wasomee humo kuna ugumu, lakini pia bweni wanalotumia wa kike na kiume ni moja ingawa limetengwa katikati na gharama zake zinachangiwa na wazazi, liko mbali na shule wakati tuna walemavu wa viungo na pia limechoka," alisema.

Kuhusu vyumba viwili vya madarasa na madawati 80 walivyokabidhiwa, alisema vitasaidia kupunguza tatizo la wanafunzi kusoma kwa awamu lililotokana na shule hiyo kuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa ya wanafunzi wasio na ulemavu.

Mwakilishi wa Meneja wa World Vision Kanda ya Kagera, George Leo, alisema mwaka 2018 walipokea maombi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ya kujengewa vyumba vya madarasa na vyoo katika shule hiyo, na mwaka 2019 walijenga matundu mawili ya vyoo ili kuwawezesha wanafunzi hasa wenye mahitaji maalumu kupata pa kujihifadhi.

"Na sasa tunawakabidhi tena madawati 80 yenye thamani ya shilingi milioni 6.4 na vyumba viwili vya madarasa, katika ujenzi huu uliogharimu shilingi milioni 62.4, wananchi wamechangia shilingi 485,000 na kiasi kilichosalia kilitolewa na World Vision kupitia ufadhili wa nchi ya Ujerumani," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Emmanuel Shelembi, alisema shirika hilo ni mdau mkubwa katika uboreshaji wa huduma za kijamii, ukiwamo ujenzi wa zahanati na vyumba vya madarasa na kuwataka kuendelea kushirikiana na serikali kuboresha maisha ya wananchi maana inatambua mchango wao.

Shule ya Msingi Kagondo 'B' ina jumla ya wanafunzi 468, idadi ambayo pia inajumuisha wa wanafunzi wa kitengo maalumu 79.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kulia), akifurahi baada ya kukata utepe kuashiri kuwashwa kwa umeme juzi katika kijiji cha Mazae Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa maji kunufaisha 16,000 Magu

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ZAIDI ya wakazi 16,000 wa Kata ya Chabula wilayani Magu mkoani Mwanza watanufaika na mradi wa maji wa Chabula-Bugando utakaotumia chanzo cha maji ya Ziwa Victoria.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, wakati wa ziara yake ya kukagua hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa mradi huo utakaonufaisha wananchi kutoka vijiji vya Bugando, Chabula, Nyashigwe na Kongolo sambamba na kuzungumza na wataalamu wanaoutekeleza.

Alisema lengo la serikali ni kuwasogezea huduma ya majisafi na salama wananchi wake ili kuwaepushia usumbufu wa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo muhimu.

"Azma ya Rais wetu ni kumtua mama ndoo kichwani kwa kumsogezea huduma ya maji ili kumwondolea kero iliyomsumbua kwa kipindi kirefu ya kutembea masafa marefu kutafuta maji," alibainisha Aweso.

Aidha, alielekeza wataalamu wanaotekeleza mradi huo kuhakikisha unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa hasa ikizingatiwa kwamba fedha ya utekelezaji wake inatoka kwa wakati.

Alibainisha kuwa Rais Magufuli ametoa zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuhakikisha mradi wa Chabula-Bugando unakamilika haraka ili wananchi wapate maji na hivyo wizara itahakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

"Tumesema sasa imetosha wananchi kuhangaika, hatuwezi tukawa na ziwa karibu hapa halafu wananchi walalamike hawana huduma ya majisafi," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kalli, alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwapatia mradi huo wa maji na alipongeza jitihada za Wizara ya Maji katika kuhakikisha miradi inajengwa kwa viwango na inakamilika kwa wakati.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Leonard Msenyele, alisema mradi unatekelezwa kwa ushirikiano wa wataalamu wa ndani kutoka Wakala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na MWAUWASA.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 9 BORA NAMBA 9 UK. 12&13



# MABEKI WA5 WALIOFUNGA MABAO MENGI MSIMU HUU

SERGIO RAMOS

## ISIKUPITE

WAKATI Manchester City wakiangukia pua kwa kipigo cha mabao 3-1 usiku wa kuamkia jana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lyon, Raheem Sterling hiyo ilikuwa mechi yake ya 50 katika michuano hiyo, huku akiwa na miaka 25 na siku 251. Mchezaji pekee wa England kufikia hatua hiyo akiwa na umri mdogo kama zaidi yake ni Wayne Rooney mwaka 2010 (miaka 24, siku 115).



**MADRID,** Hispania

NYAKATI zinabadilika. Makocha wengi kwa sasa hawataki walinzi ambao wanaweza kuzuia tu mashambulizi na kubutua mipira nje ya lango lao. Walinzi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kumiliki mpira hasa kwa walinzi wa kati.

Hata walinzi wa pembeni wanatarajiwa kuwa msaada wa kusukumiza mashambulizi mbele. Wanatakiwa kuchangia kwenye ushambuliaji kila inapohitajika kwenye mchezo.Kufunga mabao si kazi muhimu zaidi kwa mlinzi. Hata hivyo, wengine wameweza kufanya hivyo na kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja katika klabu zao.Hapa tunawaangalia walinzi watano waliofunga mabao mengi msimu huu, shuka nayo...

### #5. PHILIPP MAX, AUGSBURG | MABAO 8

Kwa sasa ana namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza na Philipp Max amekuwa akiifanya kazi yake vizuri sana anapokuwa dimbani.

Mlinzi huyu wa kushoto alijiunga na Augsburg akitokea Karlsruher SC mwaka 2015 kwa ada ya euro milioni 3.5 na amethibitisha ubora wake tangu wakati huo. Ana uwezo mkubwa wa kucheza nafasi ya mlinzi wa pembeni, lakini pia Max amekuwa na uwezo mkubwa wa kufunga na hivyo kujikuta akiwaniwa na klabu kama Manchester City, Chelsea na Lazio kwa nyakati tofauti.

Bado hajapata nafasi ya kuichezea timu ya Taifa ya Ujerumani, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amecheza mechi 31 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu uliopita. Amethibitisha ubora wake kwa kufunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita.

### #4. MARTIN HINTEREGGER, EINTRACHT FRANKFURT | MABAO 8

Martin Hinteregger Mei mwaka huu alifunga mabao mawili kwa Eintracht Frankfurt na moja la kujifunga dhidi ya Bayern Munich.

Hinteregger alijiunga Eintracht Frankfurt kutoka Augsburg kwa mkopo Januari, na baadaye akasajiliwa moja kwa moja kwa euro milioni tisa kipindi cha majira ya joto. Mlinzi huyo wa kati raia wa Austria amecheza mechi 30 na amefunga mabao nane na kutoa pasi ya mwisho moja.

### #3. DOMENICO CRISCITO, GENOA | MABAO 8

Sasa huu ni msimu wa tatu na Genoa, Domenico Criscito ndiye nahodha wa kikosi hicho.

Ni zao la akademi ya Genoa ya kulea vipaji, na nyota huyo wa kimataifa wa Italia alihamia Juventus mwaka 2004, akarudi kucheza Genoa kwa mkopo kwa kipindi cha miaka mitatu na nusu. Yakafuatia mafanikio makubwa kule Zenit Saint Petersburg, ambapo baadaye alirudi Genoa. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 33, amekuwa nguzo muhimu kwa kikosi hicho.

Criscito msimu uliopita alicheza kama mlinzi wa kati na wa kushoto kwa nyakati tofauti, akianza katika mechi 24 za Serie A. Amefunga mabao nane ya ligi pamoja na mawili kwenye Kombe la Coppa Italia.

### #2. ROBIN GOSENS, ATALANTA | MABAO 9

Atalanta ilikuwa timu inayocheza soka la kuvutia zaidi msimu uliopita kwenye Serie A, na Robin Gosens alikuwa mmoja wa nyota wake.

Gosens alihamia Atalanta akitokea Heracles Almelo kwa ada ya uhamisho ya euro 900,000 mwaka 2017 na baada ya msimu mmoja, akawa mchezaji mzuri zaidi chini ya kocha, Gian Piero Gasperini. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amekuwa akicheza kama mlinzi wa kushoto na kiungo wa pembeni.

Gosens ameanza katika mechi 31 za Serie A msimu uliopita, akifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho nane. Kiwango chake kimemfanya kuhusishwa na klabu kama Juventus na Chelsea katika miezi ya hivi karibuni.

### #1. SERGIO RAMOS, REAL MADRID | MABAO 11

Nani zaidi? Mmoja wa mabeki bora zaidi ambao mchezo huu imewashuhudia. Sergio Ramos amejiimarisha yeye mwenyewe kama mlinzi muhimu zaidi kwa kikosi cha Real Madrid na Hispania.

Ramos alijiunga na Real Madrid akitokea Sevilla mwaka 2005 kwa ada ya euro milioni 27, na hadi sasa amecheza jumla ya mechi 650 katika mashindano yote kwa klabu hiyo, akifunga jumla ya mabao 97. Ni mpigaji mzuri wa penalti, hasa baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo kumemfanya yeye kuwa mpigaji wa penalti zote za 'Los Blancos' hao.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 34, amecheza mechi 35 za Ligi Kuu msimu huu pale Real Madrid, akifunga mabao 11. Katika mashindano yote, Ramos amefunga mabao 13 kwenye mechi 44 kwa kikosi chake. Nahodha huyo wa Real Madrid, pia ni kiongozi mzuri dimbani.

## Extra Time



LUIS SUAREZ

# WACHEZAJI 9 BORA NAMBA 9

**LONDON,** England

NAMBA ya jezi imekuwa na maana kubwa mno kwa kumtambulisha mchezaji jukumu lake akiwa dimbani. Namba imekuwa na umuhimu wake na namba 9 inakuwa kwa mshambuliaji.

**Namba 9 ni mmoja wa wachezaji anayeongoza mashambulizi, anakuwa ndani ya box katika wakati maalumu na kumalizia mashambulizi. Namba 9 mara zote ni wazuri wa kuwahenyesha walinzi na 'kuwaua' magolikipa.**

Kazi ya namba 9 inahusisha kutengeneza mashambulizi mbele ya watatu wa mbele. Makala haya yanakuchambulia wachezaji tisa ambao kwa sasa ndio wanaotamba kwenye nafasi ya namba 9 duniani, twende...

### #9. LUIS SUAREZ

Luis Suarez, katika umri wake wa miaka 33, anaelekea mwisho wa kipindi chake cha uchezaji, lakini ameendelea kuwa bora mbele ya goli. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Uruguay ameisaidia Barcelona vizuri sana kwenye kucheka na nyavu.

Suarez ni namba 9 ambaye anapenda pia kutoa pasi za mwisho kwa wenzake ili kusaidia mashambulizi. Suarez amefunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 10 katika mechi 38 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu.

### #8. ROBERTO FIRMINO

Roberto Firmino ni mchezaji namba 9 wa tofauti kabisa kwenye orodha hii. Nyota huyu wa Liverpool amekuwa na upatina mzuri zaidi na washambuliaji wawili bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya England, Sadio Mane na Mohamed Salah.

Kiukweli kazi ya Firmino katika mfumo wa kikosi cha Jurgen Klopp inahitaji kufanya kazi zaidi ya kuwasaidia Salah na Mane. Firmino amekuwa kama muunganishaji mzuri zaidi kati ya kiungo na mshambuliaji.

Firmino amefunga mabao tisa kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku akitoa pasi za mwisho nane. Firmino amecheza karibia kila mchezo kwenye Ligi Kuu wakati Liverpool wakitwaa taji hilo msimu huu ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

### #7. LUIS MURIEL

Luis Muriel baada ya kujiunga na Atalanta kipindi cha majira ya joto kilichopita alicheza kama msaidizi wa Duvan Zapata.

Muriel amefunga mabao 18 kwa Atalanta wakati ikimaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Serie A. Lakini cha kufurahisha ni kwamba, ameanza katika mechi 10 tu. Ametokea benchi mara 24.

Amefunga mabao 11 yote ameyafunga akitokea benchi. Muriel ni mpiga chenga mzuri na anapenda kupiga mashuti kutoka mbali. Pia ni mpigaji mzuri wa mipira ya adhabu ndogo.

### #6. DANNY INGS

Danny Ings kwa hakika amekuwa na msimu bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na Southampton. Licha ya timu yake kumaliza nafasi ya 11 kwenye msimamo, 'watakatifu' hao walikuwa moja ya timu bora kwenye ligi, huku Ings akiwa kiongozi wa mashambulizi.

Mashabiki wa soka wa Ligi kuu England walikuwa na furaha kumuona Ings 'akifufuka' baada ya kusumbuliwa na majeraha na kuikosa misimu miwili mfululizo wakati akiwa pale Liverpool.

Hata hivyo, Ings amethibitisha ubora wake baada ya kumaliza katika nafasi ya pili ya ufungaji bora wa mabao kwenye ligi hiyo akifungana na Pierre-Emerick Aubameyang na kupitwa bao moja tu na Jamie Vardy.

### #5. ANTHONY MARTIAL

Anthony Martial amekuwa mmoja wa wachezaji walioimarika zaidi chini ya Ole Gunnar Solskjaer. Baada ya kujikuta akiwa na wakati mgumu chini ya Mourinho, Martial kwa hakika anaonyesha ishara ya kuwa mchezaji ambaye alitarajiwa kuwa.

Kwa sasa Martial anaonekana kufiti zaidi katika nafasi ya namba 9. Martial na Rashford wamekuwa wakiongoza safu ya mashambulizi ya Manchester United. Pia amekuwa akicheza vizuri sana na kinda, Mason Greenwood.

Martial amefunga mabao 23 na kutoa pasi za mwisho sita katika mashindano yote msimu huu. Kama asingekumbwa na majeruhi mwanzoni mwa msimu huu, Martial angekuwa kwenye orodha ya wanaowania Kiatu cha Dhahabu.

### #4. ROMELU LUKAKU

Romelu Lukaku amekuwa mmoja wa washambuliaji muhimu zaidi kwa Inter Milan msimu huu. Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United amekuwa na ubora wa kuvutia na amekuwa na nafasi nzuri ya kufunga mabao.

Lukaku wakati wake pale Manchester United hawezi kuhesabiwa kama alishindwa, kwani mfumo wa Jose Mourinho ulimfanya kutokuwa kwenye nafasi nzuri ya kuonyesha ubora.

Lukaku amekuwa nguzo ya mabao kwa kikosi cha Inter Milan chini ya kocha Antonio Conte. Lukaku amefunga mabao 30 katika mechi 47 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu na ametoa pasi za mwisho tano kwa jina lake.

### #3. JAMIE VARDY

Jamie Vardy amechomoza katikati ya msitu wa washambuliaji bora wa Ligi Kuu ya England na kuibuka mfungaji bora na kujitwalia Kiatu cha Dhahabu akiwa na Leicester City.

Vardy amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi hicho, kwani kasi na uwezo wake wa kufunga mabao umekuwa wa kiwango cha kuvutia sana.

Vardy ameshinda Kiatu cha Dhahabu baada ya kufunga mabao 23 katika mechi 35 alizocheza kwenye Ligi Kuu. Pia ametoa pasi za mwisho tano. Katika umri wake wa miaka 33, Vardy ameendelea kuwa mmoja wa washambuliaji wenye kasi kubwa zaidi Ulaya na ni mtu anayeibeba sana Leicester.

### #2. KARIM BENZEMA

Karim Benzema ameendelea kuwa msaada mkubwa kwa Real Madrid licha ya umri wake wa miaka 32.

Benzema amefunga mabao 26 na kutoa pasi za mwisho 10 katika mashindano yote. Ubora wake umemfanya kuendelea kuwa mshambuliaji kiongozi pale Real Madrid kwa zaidi ya muongo mmoja sasa.

### #1. ROBERT LEWANDOWSKI

Yeye ni mtu ambaye watu wengi wanaona kwamba alifaa kubeba tuzo ya Ballon d'Or ambayo msimu huu imefutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. Kwa uhakika kabisa Robert Lewandowski amekuwa ni mchezaji wa kiwango cha juu zaidi msimu huu, hasa anapokuwa jirani na goli.

Katika mechi 44 alizocheza katika mashindano yote msimu huu, Robert Lewandowski amefunga mabao 55. Hii maana yake ni kwamba amefunga zaidi ya bao moja katika kila mchezo. Bila shaka yoyote Lewa kwa sasa ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani na anaonekana ataendelea kuwa bora zaidi licha ya umri wake wa miaka 31.

Lewandowski msimu huu amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi na anaweza kuendeleza makali yake hayo hadi msimu ujao. Kwani ni wazi kabisa anaonekana hakuna wa kumzuia.

## Nukuu


"Arsenal wangependa abaki, bado hajaja na uamuzi wake, sijui nini anachofikiria, sijui Arsenal wamempa ofa gani na sizungumzii kuhusu fedha, nazungumzia kuhusu wachezaji kwa sababu wachezaji wanamtaka yeye kucheza na wale wa daraja la juu. Yeye ni mchezaji wa daraja la juu, na anataka azungukwe na wachezaji wa daraja la juu kabisa," **Robin van Persie akieleza namna ya Arsenal kuweza kumshawishi Pierre-Emerick Aubameyang kusaini mkataba mpya .**



"Kamwe sikufikiria kutolewa. Kamwe sikufikiria kurudi nyumbani, kuanzia mwanzo hadi mwisho, tulifikiria kuhusu kufuzu kwenye nusu fainali. Hakuna mtu aliyenibadilisha hilo, nataka kwenda kwenye fainali. Kiwango kingine kitakuja kwetu, sisi ni kundi kubwa, familia na akili yetu inawaza kwamba, haiwezekani sisi kutolewa," **Neymar akiiambia RMC Sport baada ya kuitoa PSG kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuichapa Atalanta 2-1.**



"Ni vizuri sana kwa watu kusema kuhusu majina hayo, lakini Cantona alikuwa wakushangaza kwa klabu hii. Ninahitaji kufanya mengi, bora zaidi kulinganishwa na yeye," **kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes akikataa kulinganishwa na nguli wa klabu hiyo, Mfaransa Eric Cantona.**






Bernard Morrison akitia dole gumba mkataba wa kuitumikia Simba: **PICHA: SIMBA**

# WAMETINGISHA USAJILI LIGI BARA KUELEKEA 2020/21

**Na Adam Fungamwango**

HARAKATI za usajili zimeendelea kupamba moto nchini Tanzania, kila timu ikisajili wachezaji ambao inaona watawafaa kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21, pamoja na mechi za kimataifa kwa timu zitakaoiwakilisha nchini.

**Kuna klabu zinaonekana kusajili wachezaji wengi kama vile wanatengeneza upya kikosi chao, lakini baadhi zinaonekana kusajili wachezaji wachache kwa ajili kile kinachoelezwa ni kuziba mapengo au mapungufu yaliyojitokeza msimu uliomalizika.**

Zipo klabu ambazo baada ya kufanya vema msimu huu zinataka kuhakikisha zinaendelea kuwa bora licha ya kuondokewa na wachezaji wao nyota, lakini klabu zilizopanda Ligi Kuu nazo pia. Ingawa bado zote 18 zinaonekana hazijamaliza usajili, lakini kuna sajili zingine ambazo tayari zimekamilika na kuthibitishwa na viongozi wa klabu.

Hizi ni baadhi ya usajili ambao tayari umekamilika, kwa wachezaji waliosajiliwa kutoka hapa hapa nchini na nje ya nchi.

**1. SIMBA**

Mabingwa watetezi Simba ambao wanakabiliwa na kibarua cha kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao yenyewe mpaka sasa imeshafanya usajili wa wachezaji Benard Morrison kutoka Yanga raia wa Ghana, Ibrahim Ally Ame (Coastal Union), Joash Onyango raia wa Kenya mchezaji huru aliyemaliza mkataba na Gor Mahia ya huko, David Kameta 'Duchu' (Lipuli), Charles Ilamfya akitokea KMC na Larry Bwalya Mzambia aliyetokea klabu ya Power Dynamos ya huko.

**2. YANGA**

Mabingwa wa kihistoria Yanga, msimu ujao hawatoshiriki michuano ya kimataifa na wanaonekana kama kujenga upya kikosi chao, wao mpaka sasa wameshawatia mikononi wachezaji Zawadi Mauya kutoka Kagera Sugar, Kibwana Shomari (Mtibwa Sugar), Waziri Junior akitokea Mbao FC, Bakari Mwamnyeto aliyetoka Coastal Union na Mustapha Yassin (Polisi Tanzania).

**3. AZAM FC**

Azam FC nayo kama Yanga haitoshiriki michuano yoyote ya kimataifa, inaonekana iko kwenye mikakati ya kuboresha kikosi chao ili kuingia na nguvu mpya msimu ujao, imewasainisha wachezaji Awesu Awesu kutoka Kagera Sugar, Emmanuel Charles (Mbao FC), David Kissu, Mtanzania aliyekuwa akikipiga Gor Mahia ya Kenya, Ally Niyonzima, Mnyarwanda aliyesajiliwa kutoka Rayon Sports ya huko, Ismail Aziz (Prisons), na Ayoub Lyanga akitokea Coastal Union.

**4. NAMUNGO FC**

Timu hii kutoka Ruangwa mkoani Lindi, imepanda na kucheza Ligi Kuu msimu huu, lakini imeleta changamoto kubwa kiasi kwamba itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Kwa sasa inafanya usajili wa 'kufa mtu' ili kupata kikosi kitakachoiwakilisha vema nchi.

Tayari imeshanasa saini za wachezaji Abdulhalim Humud kutoka Mtibwa Sugar, Steven Sey, Mghana aliyekuwa akiichezea Singida United, Fred Tangalo kutoka Lipuli na Sixtus Sabilo akisajiliwa kutoka Polisi Tanzania.

**5. KAGERA SUGAR**

Kagera Sugar imewanasa wachezaji Vitalis Mayanga kutoka Ndanda, Saadat Mohamed akitokea Ruvu Shooting, Abdallah Mfuko (KMC), Mbaraka Yusuph (Azam FC), Ally Nassor 'Ufudu' (Mbeya City), Hassan Mwaterema akitokea JKT Tanzania na Mohamed Ibrahim 'Mo' kutoka Namungo FC.

**6. DODOMA MJI**

Imepanda daraja msimu huu na itacheza kwa mara ya kwa Ligi Kuu msimu wa 2020/21, lakini tayari imeanza makeke ya usajili mapema. Imewatia mikononi Seif Karihe kutoka Lipuli, Peter Mapunda na golikipa Aron Kalambo wote kutoka Mbeya City, Cleophace Mkandara akitokea Prisons, Jukumu Kibanda (Namungo), Justine Omari (Biashara United), na Dickson Ambundo, Mbongo aliyekuwa akikipiga Gor Mahia ya Kenya, mchezaji wa zamani wa Alliance FC na Mbao FC.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO cha mabao 8-2 ilichokipata Barcelona Ijumaa usiku kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa Bayern Munich, ndicho kikubwa zaidi kwao kuwahi kukipata katika michuano hiyo, kikipiku kile cha mabao 6-2 walichokipata ndugu zao wa Hispania, Valencia kwenye Kombe la Inter-Cities Fairs, Septemba 1962. Lakini wameruhusu mabao nane katika mechi moja kwa mara ya kwanza tangu walipochapwa 8-0 na Sevilla Aprili 1946.



# Serikali yatakiwa kusaini ACDEG

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kusaini mkataba wa Afrika wa demokrasia, uchaguzi na utawala (ACDEG) kutokana na kuendana na vigezo vilivyopo kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2025.

Wakili wa kujitegemea Edson Kilatu alitoa rai hiyo jana alipokuwa akitoa mada kuhusu mkataba huo kwenye mafunzo yaliyowakutanisha waandishi wa habari na asasi za kiraia jijini hapa, yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la Serikali la ActionAid Tanzania.

Alisema miongoni mwa vigezo vinavyoendana ni maisha bora, ambapo serikali inakusudia kufikia malengo hayo kwa kutoa elimu na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Aidha, alifafanua kuwa msukumo mkubwa wa kuasisi mkataba huo ulikuwa ni kupata mwarobaini wa matatizo ya vita, mapinduzi ya kijeshi na umaskini wa kutisha uliokumba Afrika kwa miongo mingi.

"Mkataba unakataza kutwaa madaraka kwa njia zisizo za kikatiba mfano mapinduzi dhidi ya serikali halali, na unakwenda mbali zaidi kutoa jukumu kwa nchi washirika kuchukua hatua za kijeshi na kidiplomasia kunusuru nchi ikiingia kwenye hali ya kupinduliwa," alisema.

Kilatu alisema mkataba huo unaendana na katiba, sheria na sera za nchi, hivyo kwa kuuridhia hakutakuwa na mkanganyiko wowote wa kimfumo.

"Mkataba huu unatoa jukumu kwa nchi washirika kushirikiana katika kupambana na rushwa pale mtu anapokuwa amehamishia fedha au nyaraka muhimu kwenye nchi washirika na kushughulikia makosa na uhalifu mwingine," alisema.

Mbali na hayo, alisema mkataba umeanzisha mfuko wa kuwezesha na kujengea uwezo tume za uchaguzi jambo ambalo ni faida kwa Tanzania.

"Mkataba unatoa mwongozo wa namna chaguzi zinatakiwa kuendeshwa pamoja na mifumo bora ya taasisi za kusimamia uchaguzi," alisema.

Pia alisema mkataba unaruhusu mgombea binafsi kama sehemu ya kupanua wigo wa kidemokrasia pamoja na haki ya kuhoji matokeo ya uchaguzi.

"Suala la mgombea binafsi na kuhoji matokeo ni mambo pekee ambayo katiba yetu bado haijaruhusu pamoja na kwamba nchi karibu zote zinatuhusu kuhoji matokeo, nchi nyingi zimeruhusu mgombea binafsi," alisema.

Hata hivyo, alisema mkataba huo unatoa fursa kama kuna vipengele nchi haikubaliani navyo inaomba vikae pembeni kwa muda.

"Watanzania wanahitaji mkataba huu ambao umeshasainiwa na nchi 45 kati ya 55 za Afrika, naamini serikali yetu itaona umuhimu wa kuridhia mkataba huu," alisema.

Naye, meneja wa masuala ya kilimo na ardhi wa ActionAid Tanzania, Elias Mtinda, alisema mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kupata uelewa kuhusu mkataba huo na kuwa na sauti ya pamoja.

Alisema mkataba huo sio mbaya kwa kuwa vigezo vingi vinatekelezwa na serikali, na hivyo hakuna kitu kinachosababisha usisainiwe.



Vijana wakivuna bamia kwenye shamba lao mwisho wa wiki katika Kijiji cha Mtumbulu Wilaya ya Dodoma mkoani humo. Kilimo hicho kinawasaidia vijana kujiajiri pamoja na kuajiri wengine. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viongozi wa mitaa wapewa jukumu kuunganisha umeme

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amewataka viongozi wa serikali za mitaa kuwahamasisha wananchi wao kulipia ili waunganishiwe huduma ya umeme.

Mgalu alitoa ushauri huo juzi katika ziara ya ukaguzi ya kazi ya usambazaji umeme vijijini kwenye kijiji cha Mazae, Wilaya ya Mpwapwa, kabla ya kuwasha umeme katika Shule ya Msingi ya Mazae kijijini hapo.

Naibu Waziri huyo alisema hajaridhishwa na kasi ya uunganishwaji wa umeme katika kijiji hicho, na kuwataka viongozi hao kufanya mikutano ya kuhamasisha wananchi wa maeneo yao kulipia huduma ya umeme ili wanufaike na huduma hiyo.

"Serikali inatumia gharama kubwa kuwafikishia umeme hapa, lakini baadhi ya maeneo huduma ya umeme imefika wananchi bado hawajalipia ikiwamo hapa Mazae," alisema.

Alitaja maeneo mengine ni pamoja na Isomvu, Chungu, Darajani na Nyabu.

"Serikali imepunguza gharama ya kuunganisha umeme vijijini ambayo ni 27,000 tu huu mradi unakaribia kufika ukingoni wananchi wanaonekana hawajalipia na mkandarasi amesema kuwa wananchi wakilipa yeye yupo tayari kuwaunganishia kwa hiyo niwaombe wananchi wapo kwenye wigo maeneo ambayo mradi umefika mlipie ili mpata kunganishiwa umeme," alisema.

Aidha, alibainisha kuwa serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma ya umeme na tayari imeingia katika utekelezaji REA III mzunguko wa pili.

"Pia kuna mradi mwingine wa ujazilishi ambao Mkoa wa Dodoma upo kwenye miradi hiyo hivyo wananchi mnatakiwa kuchangamkia fursa hiyo ili iwasaidia katika kujiendeleza kimaendeleo katika maeneo yao," alisema.

Kadhalika, alisema miradi mingi nchini inatekelezwa bila ya elimu ya kutosha kwa wananchi jambo linalochelewesha kutambua umuhimu wake.

"Zaidi ya Sh. bilioni 800 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya usambazaji umeme ambapo kuanzia Agosti 20 hadi Septemba mwaka huu, serikali itakuwa inakabidhi kazi ya usambazaji umeme kwenye vijiji na vitongoji nchini kwa makandarasi wapya," alisema.

Aliwataka wananchi ambao vijiji na vitongoji vyao havijafikiwa na miradi ya umeme kutokuwa na hofu kwa kuwa utekelezaji wake unaendelea.

"Tayari serikali imeshapeleka umeme kwenye vijiji takriban 9,512," alisema.

Naye Mkazi wa Mazae, Hamis Israel, alishukuru serikali kwa kupeleka huduma hiyo ambayo itasaidia kujikwamua kiuchumi.

# Katibu mkuu azipa siku 14 taasisi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, ameagiza ifikapo Agosti 30, mwaka huu wakurugenzi wa taasisi zilizo chini yake zinazohusika na mbunifu wa mashine ya kuchakata katani kukutana ili kuweka mazingira ya kufanya kazi naye.

Taasisi hizo ni ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO).

Prof. Shemdoe alitoa agizo hilo kufuatia maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, hivi karibuni ya kutaka mbunifu Daudi Magari atambulike na kazi yake iwekwe jina lake.

Alisema utekelezaji wa agizo hilo umeanza na kutoa muda hadi Agosti 30, mwaka huu taasisi hizo zikutane na mbunifu huyo kwa ajili ya kumuinua na kutangaza kazi zake.

Alisema lengo la wizara hiyo ni kuwainua wabunifu kupitia kazi wanazofanya ili zitambulike ndani na nje ya nchi.

"Tunataka kuona wabunifu na kazi zao wanatambuliwa na serikali Wizara ya Viwanda imetambua wabunifu wengi na itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha wabunifu wote wanatambulika kitaifa, "alisema.

Alimtaka mbunifu huyo kuwafundisha ubunifu vijana wanaochipukia katika fani hiyo ili Tanzania kuwe na wabunifu wa kutosha.

Kwa upande wake, mbunifu huyo alilishukuru Shirika la Oxfam Tanzania ambao waliona kazi yake na kuamua kuitangaza kwa kupeleka kwenye maonyesho mbalimbali.

Alisema kazi ya ubunifu anaifanya vizuri isipokuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa vifaa ambayo wakifanikiwa kuitatua basi itakuwa rahisi kufanya kazi zao.

Naye Mratibu wa Fedha wa Shirika la Oxfam Tanzania, Cecilia Makota, alisema shirika hilo litaendelea kuibua vipaji vya wabunifu mbalimbali ili watambulike na serikali.

"Hatutachoka kuendelea kuibua wabunifu kwa sababu tunahitaji kuona Tanzania ya viwanda inazidi kukua," alisema.



# TAKUKURU kupambana na taasisi zinazotoa mikopo

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia mstaafu Nicodemas Mwangela, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kutokomeza taasisi zinazotoa mikopo kwa wananchi bila kuwa na vibali.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki, wakati alipokuwa anamkabidhi Mwalimu mstaafu Aston Nzunda, mkazi wa Mbozi Mission, Sh. 7,000,000, kati ya milioni 10 ambazo ziliokolewa na TAKUKURU kutoka kwenye taasisi ambayo ilimkopesha kwa riba kubwa.

Alisema taasisi zinazotakiwa kubaki ni zile zilizosajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ama zilizosajiliwa na Wizara ya Fedha na Mipango na zingine zote zinatakiwa ziondolewe ili kuwaepusha wananchi kudhulumiwa mali zao.

"TAKUKURU mnatakiwa kufanya kazi ya kutoa elimu kwa wananchi ili wajue maeneo sahihi ya kwenda kukopa fedha na kuachana na mikopo ya mitaani ambayo inawaumiza, hapo tutakuwa tumewasaidia wananchi wetu," alisema Brig. Mwangela.

Aliwataka wananchi wengine ambao wametozwa riba kubwa kwenye mikopo hiyo ya mitaani kupeleka taarifa kwenye vyombo vya dola ili wasaidiwe kuokoa fedha zao.

Awali, akikabidhi fedha hizo, Mkuu wa TAKUKURU wa mkoa huo, Damas Suta, alisema katika kipindi cha miezi miwili taasisi hiyo iliokoa Sh. milioni 15 kupitia operesheni tokomeza mikopo umiza ambayo ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli.

Alisema mbali na Sh. milioni 10 za Mwalimu Nzunda, pia Sh. 5,000,000 ziliokolewa katika Wilaya ya Ileje ambazo zilikuwa za Mwalimu Leah Masamba, ambaye pia alikuwa amekopeshwa fedha na moja ya taasisi na kutozwa riba kubwa.

Alisema Mwalimu Nzunda alikopeshwa Sh. 8,000,000, ndani ya miezi mnane alitakiwa kulipa Sh. milioni 25 na Mwalimu Masamba alikopeshwa Sh. 1,000,000 na akatakiwa kulipa Sh. 5,000,000.

# Ataka mashine kupimia VVU kupelekwa Songwe

**Na Nebart Msokwa, MBOZI**

KATIBU Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Doroth Mwaluko, ameagiza uongozi wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), kupeleka mashine ya kupimia wingi wa virusi vya UKIMWI (VVU) kwenye damu za watu wanaoishi na virusi hivyo mkoani Songwe ili kurahisisha upimaji.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua miradi ya vikundi vya watu wanaoishi na VVU Konga ya Mbozi, mkoani Songwe na kuwataka viongozi hao kutekeleza agizo hilo ndani ya wiki mbili.

Doroth alitoa agizo hilo kufuatia taarifa ya Mganga Mkuu, Dk. Hamad Nyembea, kuonyesha kuwa mkoa huo unashindwa kutimiza moja ya 95 kati ya tatu kwenye vita dhidi ya UKIMWI ambayo ni kufubaza VVU kwa watu wanaotumia dawa.

Dk. Nyembea alisema kutokana na mkoa huo kutokuwa na mashine hiyo, wanalazimika kutuma sampuli za damu mkoani Mbeya ambako ndiko zilipo hali ambayo inasababisha kuchelewa kupata majibu.

Alisema mpaka mwezi Juni 30, mwaka huu, mkoa huo ulifikia asilimia 83 ya kuwatambua watu wanaoishi na VVU na asilimia 99 ya waliobainika kuwa na maambukizi wameingizwa kwenye matumizi ya dawa za kufubaza virusi.

"Tatizo linalotukabili ni ukosefu wa mashine ya kupimia wingi wa VVU kwenye damu, tuliomba mashine hii kwa muda mrefu na tukaahidiwa kuletewa, lakini mpaka sasa hatujaletewa licha ya maandalizi kukamilika, hivyo tunaomba tusaidiwe," alisema Dk. Nyembea.

Katibu Mkuu alimtaka Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, kutoa sababu ya mkoa huo kukosa mashine hiyo kwa maelezo kuwa alishapata taarifa muda mrefu kuwa zimeshanunuliwa.

Dk. Maboko alikiri mashine hizo kununuliwa na kwamba moja ya mikoa iliyokuwa inapewa kipaumbele kupatiwa ni Mkoa wa Songwe ambao ulitakiwa upatiwe mbili na moja iwekwe katika mji wa Tunduma na nyingine katika mji wa Mlowo.

Alisema alikuwa hana taarifa kuwa mashine hizo bado hazijapelekwa katika mkoa huo na kuahidi kufuatilia na kuhakikisha zinaletwa haraka ili kuuwezesha mkoa huo kutekeleza kwa ufanisi mapambano dhidi ya UKIMWI.

"Nikishatoka hapa Katibu Mkuu, nitawapigia simu wasaidizi wangu ili kujua sababu za mashine hiyo kutoletwa hapa na nakuhakikishia ndani ya muda mfupi italetwa," alisema Dk. Maboko.

Baada ya maelezo Dk. Maboko, Katibu Mkuu Mwaluko, alimtaka kuhakikisha mashine hiyo inapelekwa mkoani humo ndani ya wiki mbili, huku akisisitiza kuwa atafuatilia ili kujua kama agizo hilo limetekelezwa.

"Kama gari ya kusafirishia mashine hiyo haipo, mtasafirisha hata kwa ndege ili wakaipokee katika Uwanja wa Kimataifa wa Songwe, vinginevyo kila mtu ana mnyonge wake," alisema Mwaluko.

Alisisitiza kuwa Mkoa wa Songwe ni miongoni mwa iliyo na maambukizi yanayoongezeka kwa kasi na kwa sasa ni asilimia 5.8 kiwango ambacho ni zaidi ya kile cha kitaifa.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu Mwaluko alipiga marufuku matumizi ya neno 'unyanyapaa' kwenye kampeni za UKIMWI kwa kuwa inawafanya watu wanaoishi na VVU kujinyanyapaa wenyewe.

Aliagiza TACAIDS wabuni msamiati mwingine ambao utakuwa unachapishwa hata kwenye mabango na fulana.




Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Doroth Mwaluko (katikati), akizungumza na wanachama wa kukundi cha watu wanaoishi na VVU, kulia ni Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko na kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# H'shauri yaagiza wachambua chupa dambo kuondolewa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imeagizwa kuwaondoa wananchi wanaofanya kazi ya kuchambua chupa za plastiki kwenye dampo la jiji hilo lililopo katika Kata ya Nsalaga kwa kuwa kitendo hicho ni ukiukwaji wa taratibu za uhifadhi wa taka. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mazingira, Musa Sima, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua dampo hilo na kukuta baadhi ya wananchi wakiendelea kutenganisha taka.

Alisema ni kinyume cha taratibu za utunzaji wa taka, lakini ni hatari kwa afya za wananchi hao kwa kuwa wanaweza wakapata maambukizi ya magonjwa.

Naibu Waziri Sima, alisema wananchi hao pia wanasababisha taka hizo kusambaa nje ya dampo hilo na kuwa kero kwa wananchi wanaoishi jirani.

"Tunazitoa taka kwenye makazi ya wananchi ili kuwalinda na magonjwa, lakini hapa tumewaruhusu tena wananchi hao hao wanaingia humu, sasa naagiza muwaondoe haraka sana, hawawezi wakawa wanatufundisha kuchambua taka," aliagiza Naibu Waziri Sima.

Alisema kama wanataka wachambua chupa hizo, wanatakiwa wafanye kazi hiyo kabla taka hizo hazijapelekwa kwenye dampo hilo. Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Ndeleka Vanika, alisema taka hizo hukusanywa na vikundi vya wananchi katika ngazi ya kata na kuzipeleka hadi kwenye maghuba na halmashauri huzizoa na kuzipeleka kwenye dampo hilo bila kuzitenganisha.

Alisema wananchi huingia ndani ya dampo na kuzitenganisha kwa kuchukua taka za plastiki hasa chupa na kwenda kuziuza.

Kwa siku halmashauri hiyo husafirisha taka zenye uzito wa tani 175 sawa na asilimia 65 ya taka zote zinazozalishwa katika jiji hilo na kwamba katika ngazi ya kata ukusanyaji husimamiwa na viongozi wa kata husika ambao pia ndio wanaofanya kazi ya kukusanya kodi. "Ukusanyaji wa taka huanzia kwenye ngazi ya kata ambako hukusanywa na kupelekwa kwenye maghuba ambayo yapo katika kila kata, taka hizo huwa zinasafirishwa kuletwa hapa bila kutenganishwa na ndio maana hawa wananchi wanashawishika kuja kuchambua," alisema Vanika.

Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof. Esnali Sinde, alisema kitendo cha wananchi kuingia kwenye dampo kutenganisha taka, kinaaingizia serikali hasara na kuagiza kazi hiyo ifanyike nje ya dampo.

Alisema serikali inaingia hasara kwa sababu mashine inayosaga taka hizo inashindwa kufanya kazi kwa ufasaha wakati wananchi wakiwa wanaendelea kuchambua taka hizo.

## HABARI ZANZIBAR





Wakazi wa Kijiji cha Nyazwa, Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa wakimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi (kulia), zawadi ya mbuzi baada ya kufanya ziara ya kusikiliza kero zao kupitia mikutano ya hadhara maarufu kama mahakama ya wananchi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Vijana kuwezeshwa kuongeza kipato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KITUO cha kukuza na kulea wajasiriamali Zanzibar kimeandaa shindano la mpango wa biashara lenye lengo la kuongeza kipato kwa vijana.

Mkurugenzi wa Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ameir Haji Sheha, alisema kuwa shindano hilo litajumuisha vijana kutoka Zanzibar ambao watawasilisha mawazo yao.

Alisema baada ya kupokea mawazo hayo kutakuwa na mchujo na kuchagua mawazo ya watu 30 ambayo yatakuwa endelevu, yenye tija na yenye kutekeleza.

Sheha alisema kuwa vijana hao watapatiwa mafunzo ya wiki mbili juu ya uandikaji wa mpango wa biashara katika kituo hicho. Aidha, Mkurugenzi huyo alieleza kwamba katika mawazo hayo washindi watano wa mwanzo watapatiwa zawadi na kupatiwa nafasi katika kituo hicho kwa miezi mitatu, ili kusaidiwa kutekeleza mawazo yao.

Ofisa Mafunzo wa Mradi huo, Asha Nassir Salum, alisema kuwa mradi huo umelenga katika maeneo manne makubwa yakiwamo afya, elimu, teknolojia na kilimo.

Alisema wamejipanga vizuri katika shindano hilo ambalo ni la Zanzibar nzima na matarajio yao ni kuona kijana anakuwa na kampuni yake mwenyewe ambayo ataweza kuajiri na wenzake.

"Tumekuwa na utaratibu wa kuandaa shindano hilo kila mwaka, lakini mara nyingi huwashirikisha vijana waliohitimu vyuo vikuu, ingawa mara hii ni kwa wajasiriamali wote," alisema. Tangu kuanzishwa kwa kituo hicho ambacho ni miaka mitano sasa, kuna kampuni ndogo zaidi ya 70 ambazo wametokana na kituo hicho, ambapo kupitia shindano hilo maombi 20 yameshawasilishwa.

Mradi wa shindano la mpango wa biashara unatarajiwa kutumia Sh. milioni 50, fedha ambazo zimetolewa na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) na utatekelezwa kwa miezi sita, ambapo maombi ya kushiriki kwenye shindano hilo yalianza Julai 25 hadi Agosti 31, mwaka huu.

# Wanafunzi wa ualimu watakiwa ubunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wa fani ya ualimu kuhakikisha wanakuwa wabunifu ili taifa lizalishe wasomi imara.

Akizungumza katika mahafali ya 14 ya Chuo cha Kiislamu Mazizini (CCK) Mjini Unguja, alisema ni vyema walimu kuitendea haki fani yao kwa kuhakikisha kiwango cha ufaulu kinaongezeka nchini.

Aidha, aliwataka wahitimu hao watakapokuwa katika majukumu yao kuhakikisha wanawafundisha watoto masuala ya uzalendo wa nchi yao ili nao watakapohitimu wawe mstari wa mbele kutetea taifa lao popote duniani.

Waziri huyo aliwataka walimu na wahitimu hao kuhakikisha wanapinga vitendo vyote vya udhalilishaji ili kujenga jamii yenye maadili mema.

Riziki pia aliwataka wa chuo hicho kukubali mabadiliko ya elimu serikali itakapoamua kukiunganisha na Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kwa lengo la kutanua zaidi taaluma mbalimbali nchini. Pia, aliwataka vijana kutimiza wajibu wao wa kupiga kura wanapotimiza sifa za Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na kuwasisitiza kudumisha amani wakati wote ili maendeleo yaweze kupatikana.

Naye Katibu Mkuu Wizara hiyo, Idrisa Muslim Hija, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ipo katika mchakato wa kukipandisha hadhi Chuo cha Kiislamu Zanzibar kufikia ya kimataifa kwa kukiunganisha na SUZA.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Idara ya Mafunzo ya Ualimu Maimuna, Fadhil Abas, aliwataka wahitimu wa chuo hicho kuhakikisha wanatoa taaluma waliopatiwa kwa weledi ili taifa lizalishe wataalamu wake waliobobea.

Mkuu wa chuo hicho, Bakar Chum Ame, aliipongeza Wizara ya Elimu Zanzibar kwa kuhakikisha chuo hicho kinapata hatimiliki ya eneo lao pamoja na kujengewa uzio ili kuendelea kutoa taaluma katika mazingira salama.

Mwanafunzi Juma Haji Silima akisoma risala kwa niaba ya wenzake, alisema watatumia taaluma waliyopata kwa kuitumikia nchi na kuonyesha mwonekano mpya wa kuleta maendeleo katika sekta ya elimu hasa upande wa utoaji taaluma kwa wanafunzi ili kujenga jamii bora.

Jumla ya wanafunzi 539 walihitimu masomo yao katika fani za sayansi, sanaa, elimu ya maandalizi msingi awali, mafunzo maalum ya walimu wa maandalizi na elimu ya sekondari NECTA katika ngazi ya stashahada na cheti.

# Serikali yajizatiti watoto kusomea mazingira mazuri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Rais ya kutafuta madawati ya shule za serikali Zanzibar, Haroon Ali Suleiman, amesema lengo la serikali ni kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma katika mazingira mazuri na yenye kuridhisha.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi madawati katika Shule ya Dk. Salmin Amour Juma huko Chumbuni Mjini Unguja, alisema ni fursa ya kila raia kupata haki yake ya msingi ya elimu, na kuwa serikali imekuwa ikihakikisha inapatikana bure kuanzia maandalizi, msingi na sekondari katika mazingira mazuri.

Haroun ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), alisema elimu bure lazima iende sambamba na mazingira mazuri kwa watumishi wote, hivyo ana imani kuwa walimu wataongeza bidii ya ufundishaji kutokana na kuwapo mazingira mazuri ya kufundishia.

Aidha, aliwaomba wananchi kuunga mkono juhudi kubwa za serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinazofanywa katika nyanja mbalimbali hasa za kielimu kwa kuwahamasisha vijana wao kusoma ili malengo ya serikali ya kuwa na wataalamu wake yaweze kufikiwa.

Haroun aliutaka uongozi wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum na Vikosi vya SMZ, kuhakikisha wanayawekea alama maalum madawati yote na kuhakikisha hayatumiki kinyume cha malengo yaliyokusudiwa ili yasipotee na yadumu kwa muda mrefu na kuwasaidia watoto wao.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, ambaye ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema ushirikiano kati ya kamati ya madawati na Wizara ya Elimu ni miongoni mwa njia za mafanikio ya kupunguza tatizo la madawati nchini.

Aliwataka viongozi wa halmashauri kushirikiana na walimu wa shule za msingi kuhakikisha madawati hayo yanagawiwa kwa wakati ili lengo la kupunguza tatizo la madawati litimie.

Naibu Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji wa wizara hiyo, Abdullah Mzee Abdullah, alisema ni agizo la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein la kutafuta madawati ili kuhakikisha tatizo hilo linapungua na kila mwanafunzi anasoma katika mazingira mazuri na ya kuridhisha.

Jumla ya makontena tisa yenye madawati 4,495 kwa ajili ya wanafunzi wa madarasa ya msingi yalikabidhiwa katika awamu ya tatu.

# Barabara inayounganisha daraja Nyerere kukamilika

**Na Mwandishi Wetu**

UJENZI wa barabara inayounganisha daraja la Nyerere, Kigamboni upo katika hatua ya mwisho na kutatua changamoto za usafiri katika eneo hilo.

Hayo yalibainika jana wakati wa ziara ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, na viongozi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Aidha, baadhi ya wananchi wa eneo hilo wamepongeza kukamilika kwa ujenzi huo na kwamba utarahisisha usafiri, huduma za kijamii na kuongeza kasi ya maendeleo.

Meja Mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kutoka Kamandi ya Navy, Adiel Raphael Kaaya, alisema mradi wa barabara ni mkubwa na mzuri kutokana na kujengwa katika viwango vya hali ya juu.

Naye dereva wa bodaboda, Godfrey Kurumwa, alisema barabara hiyo imetengenezwa kwa ubora na viwango vya hali ya juu na hakuna haja ya kumshawishi mtu kuona kazi inayofanyika.

Naye Mkazi wa Kigamboni, Simon Robert, alisema kukamilika kwa barabara hiyo kutawaondolea adha ya muda mrefu wananchi kwa sababu barabara iliyokuwapo mwanzo ilikuwa mbovu na nyembamba.

Awali, akizungumza na wananchi wa Kigamboni, Waziri Mhagama alisema ujenzi wa barabara hiyo utafungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa wananchi na kwamba inatarajiwa kukabidhiwa Agosti 31, mwaka huu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kukamilika kwa ujezi na kwamba yanayofanyika ni matokeo ya maelekezo yake baada ya mwamko wa muda mrefu wa kipande hicho cha barabara.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (mwenye kitenge), akikagua ujenzi wa barabara inayounganisha daraja la Mwalimu Nyerere na makazi ya watu Kigamboni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Machinjio Vingunguti kukamilika Oktoba

**Na Mary Geofrey**

UJENZI wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti, umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, mwaka huu na kuanza kutumika rasmi.

Kwa sasa kazi inayoendelea ni kusimika mashine na mitambo mbalimbali ikiwamo ya kuchinja ng'ombe na kupooza nyama inayochinjwa.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Joseph Nyamhanga, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara katika machinjio hayo ili kufahamu maendeleo ya mradi huo wa kimkakatii.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kapatikana kwa nyama yenye ubora ikilinganishwa na machinjio ya awali na kupatikana kwa ajira za kudumu 300 na za muda 3,000.

Alisema pia machinjio hayo itakayokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 3,000 kwa awamu tatu kwa siku, itawezesha kukusanya mapato ziadi ya Sh. bilioni 3.4 kwa mwezi. Aliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, kumtafuta msimamizi wa mradi huo pamoja na kuandaa utaratibu wa aina ya ng'ombe wa kuchinja watakaokuwa na ubora unaokubalika.

Pia alitembelea mradi wa soko kuu la kisasa la Kisutu na kuagiza mkandarasi kukamilisha ujenzi wake ndani ya miezi miwili.

Aliiagiza pia halmashauri ya wilaya hiyo, kuanza kufanya maandalizi ya uendeshaji wa soko hilo ili litakapokamilika lianze kufanya kazi haraka.

# Masoko ya madini yachangia kuongezeka mapato

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Robert Luhumbi, amesema masoko ya kuuzia madini ya dhahabu mkoani humo yamechangia kuongezeka kwa mapato yatokanayo na sekta ya madini na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini kupeleka nje ya nchi.

Luhumbi alitoa kauli hiyo jana wakati wakiwahutubia wananchi wa Wilaya ya Nyang´hwale, kwenye hafla fupi ya kufungua soko la kuuzia madini ya dhahabu, wilayani hapo.

Alisema kabla ya kuwapo kwa masoko ya kuuzia madini ya dhahabu hali ya ukusanyaji wa mapato ilikuwa mbaya, mwaka 2019 soko kuu la madini Geita lilipofunguliwa rasmi na Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa na kununua madini ya dhahabu mapato ya serikali yameongezeka kutoka Sh. milioni 600 kwa mwezi na kufikia Sh. bilioni 44.

Kadhalika, alisema makusanyo hayo ni tozo ya mrabaha wa serikali kutoka kwa wachimbaji wadogo na madini ya dhahabu yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 55.8 yameuzwa katika soko kuu la Geita kwa kipindi cha miezi miwili iliyopita na serikali kupata kodi yake kutokana na kudhibiti mianya ya utoroshwaji wa madini hayo.

"Masoko ya madini yamedhibiti mianya ya utoroshaji wa madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu na kuongeza makusanyo kodi ya serikali tangu kuanzishwa masoko hayo katika mkoa wa Geita kuna jumla ya masoko madogo ya kununua na kuuzia dhahabu tisa na soko kuu la madini Geita.

Ofisa Madini Mkazi Geita, Daniel Mapunda, akitoa taarifa wakati wa ufunguzi wa soko hilo, alisema Mkoa wa Geita una utajiri mkubwa wa madini ya dhahabu karibu kila wilaya hiyo una masoko madogo ya kuuzia madini, likiwamo soko jipya la Nyanghwale.

Alisema kabla ya masoko ya madini kuanzishwa mapato kwa mwezi yalikuwa Sh. milioni 600, lakini baada ya masoko kujengwa katika wilaya za mkoa huo mapato kwa mwezi yamepanda na kufikia zaidi ya Shilingi bilioni tatu kwa mwezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Marim Chaurembo, alisema asilimia 70 ya mapato ya ndani katika halmashauri hiyo yanatokana na wawekezaji waliowekeza sekta ya madini na ujenzi wa soko hilo umegharimu Sh. milioni 700.

## Simbachawene avionya vyama kuelekea uchaguzi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama nchini kudhibiti vyama vya siasa vitakavyofanya siasa kinyume na sheria na kusababisha uvunjifu wa amani kwa wananchi.

Simbachawene aliyasema hayo jana mkoani Kigoma, wakati wa ziara yake ya kwanza mkoani humo tangu kuchaguliwa katika nafasi hiyo na kuviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuanzia ngazi ya kata hadi taifa, kuwadhibiti wanasiasa wanaofanya siasa zenye viashiria vya chuki ili kulinda maisha ya Watanzania wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Alisema uchaguzi huu ni wa awamu ya sita tangu mfumo wa demokrasia wa vyama vingi uanze kutumika nchini mwaka 1995, hivyo hategemei kusikia Mtanzania yeyote kupoteza maisha katika mchakato huo kwa kuwa mfumo huo sio mpya nchini.

"Naomba nivionye vyama vya siasa vyote vyenye wagombea katika ngazi mbalimbali vizingatie sheria na kubeba jukumu la kila wanachokifanya kutoleta uvunjifu wa amani," alisema.

Vile vile, katika ziara hiyo mkoani humo imejikita kutafuta suluhu ya kufanikisha wakimbizi kurejea nyumbani kwao kwa kuwa mpango uliowekwa awali wa urejeshwaji wa hiari kama mikataba ya kimataifa inavyosema kutofanikiwa na hadi sasa nchi ina hifadhi wakimbizi 288,758.

Naye Mkurugenzi Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, Sudi Mwakibasi, alisema wanakambiliwa na changamoto ya uwezo mdogo wa nchi ya Burundi kupokea wakimbizi baada ya kupanga kila wiki kurejesha watu 400 na kusababisha zoezi hilo kuwa gumu na kushindwa kufikia lengo.

# Wapiganaji wenye itikadi waiteka bandari

**MAPUTO,** Msumbiji

HALI ya usalama Kaskazini mwa Msumbiji inazidi kuwa mbaya baada ya wapiganaji wenye itikadi kali kuiteka bandari iliyopo katika Bahari ya Hindi.

Vikosi vya usalama vya Msumbiji juzi, vilipambana na wanamgambo wenye itikadi kali za Kiislam ili kurudisha tena udhibiti wa bandari muhimu katika jimbo lenye utajiri wa gesi kaskazini mwa Msumbiji.

Waziri wa Ulinzi wa Msumbiji, Jaime Neto, aliyasema hayo jana ikiwa ni siku moja baada ya bandari katika mji wa Mocimboa da Praia kutekwa na wapigananaji wenye itikadi kali mapema asubuhi jana.

Wanamgambo hao pia wanasemekana kuwa na uhusiano na Afrika Kusini. Mnamo Agosti, 2018, mamlaka ya Msumbiji ilimkamata raia mmoja wa Afrika Kusini, André Mayer Hanekom, anayejulikana ambaye alihusika na kuwapelekea waasi silaha, dawa na pesa ambazo ziliwawezesha kulipa mishahara ya wapiganaji wao.

Mayer alifariki akiwa chini ya ulinzi wa polisi Januari mwaka 2019 katika hali isiyoeleweka.

Taarifa za ndani kutoka Msumbiji zinaeleza kuwa kutekwa kwa Bandari ya Mocímboa da Praia na waasi hao inamaanisha kwamba vikosi vya serikali kwa sasa vimeshindwa kuwadhibiti wanamgambo. Mtaalamu wa masuala ya kisiasa nchini Msumbiji, Dércio Alfazema, alisema katika sehemu ya nchi, kwenye mkoa wa Cabo Delgado, kuna uwekezaji mkubwa zaidi katika sekta ya malighafi barani Afrika kote.

Alisema Mocímboa da Praia iko umbali wa kilomita 90 tu kutoka kwenye mradi wa mkubwa wa gesi asilia unaozihusisha kampuni za Ufaransa, Marekani, Italia na kampuni zingine za nishati.

Alisema serikali ya Msumbji haitawapa nafasi magaidi kudhibiti eneo lolote nchini humo na kuongeza kwamba haitakubalika kamwe eneo la Cabo Delgado litumbukie katika hali ya machafuko na ukiukaji wa haki za msingi za binadamu.

Alisema vijiji vingi vimeteketezwa na ambao wameshindwa kukimbia wanakabiliwa na viitisho vya mara kwa mara au hata kuuliwa.

Katika siku chache zilizopita, familia nyingi zimekimbia kutoka kwenye eneo hilo kwa kuvuka bahari, au kwa kutumia mabasi, kupitia kwenye mpaka wa Pemba, katika mji wa Cabo Delgado.

Kulingana na takwimu za Umoja wa Mataifa (UN), zaidi ya watu 1,500 wameuawa na wengine wapatao 250,000 wamekimbilia sehemu zingine za nchi.

Mashambulio hayo yalianza mnamo 2017 huko Mocimboa da Praia na kuenea kwenye maeneo makubwa ya Cabo Delgado. **DW**

# Marekani yashindwa kuongeza muda wa vikwazo silaha Iran

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imeshindwa kupata ridhaa ya kuongeza muda wa vikwazo vya silaha dhidi ya Iran, vinavyofikia ukingoni.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, amelikosoa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN), kwa kushindwa kutekeleza jukumu lake la kuendeleza usalama na amani ya kimataifa.

"Imekataa kuongeza muda wa azimio la marufuku ya silaha dhidi ya Iran ambalo limekuwapo kwa miaka 13, kutoa mwanya kwa Taifa linaloongoza kufadhili ugaidi kununua na kuuza silaha bila ya kuwapo masharti ya UN kwa mara ya kwanza katika zaidi ya muongo mmoja," alisema Pompeo na kuongeza:

"Kushindwa kwa Baraza la Usalama kuchukua maamuzi muafaka kulinda usalama na amani ya kimataifa hakukubaliki hata kidogo," alisema Pompeo.

**Katika historia ya miaka 75 ya UN, Marekani haijawahi kutengwa kama hivi leo.**

Azimio la Marekani liliungwa mkono kwa kura mbili za Marekani na Jamhuri ya Dominica.

Russia na China zilipiga kura kupinga hatua ya vikwazo hivyo, na nchi nyingine 11 wanachama wa baraza hawakupiga kura. Balozi wa Iran katika UN, Majid Takht Ravanchi, alisema vikwazo vyovyote au masharti yoyote yale yatakayowekwa na Baraza la Usalama, yatajibiwa kwa hatua kali.

Msemaji wa Mambo ye Nje ya Iran, Abbas Mousavi, kupitia akaunti ya kijamii ya Twitter aliandika kuwa: "Katika historia ya miaka 75 ya UN, Marekani haijawahi kutengwa kama hivi leo."

Aliongeza: "Pamoja na safari zote walizofanya, shinikizo walilolweka na ubabe wa kivita, Marekani iliweza tu kuihamasisha nchi ndogo kupiga kura pamoja nayo."

"Jana usiku, diplomasia ya Iran inayofanya kazi, pamoja na nguvu ya sheria ya mkataba wa nyuklia, imeishinda Marekani kwa mara nyingine katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa."

Ofisi ya ubalozi wa China katika UN imetuma ujumbe unaoeleza kuwa: "Ubinafsi hauwezi kuungwa mkono, na ubabe hautafanikiwa. Jaribio lolote la kuweka maslahi binafsi juu ya maslahi ya wengi ya jumuiya ya kimataifa yatagonga ukuta."

Marufuku dhidi ya uuzaji au uhamishaji wa silaha za kawaida, kusafirishwa kwenda Iran au kutoka Iran unafikia ukomo ifikapo Oktoba, 18 chini ya mkataba kamili wa Mpango wa Utekelezaji (JCPOA). **VOA**



Polisi mjini Bangkok wakijaribu kuwazuia waandamanaji kuufikia mnara wa demokrasia wakati wa maandamano nchini Thailand. **PICHA: DW**

# Waandamana kuipinga serikali

**BANGKOK,** Thailand

MAELFU ya waandamanaji walikusanyika mjini Bangkok wakipaza sauti dhidi ya serikali ya nchi hiyo, wakati mivutano inaongezeka katika Taifa hilo la kifalme, barani Asia.

Vuguvugu la kudai demokrasia limeshika kasi nchini Thailand, nchi hiyo imeshuhudia maandamano kila siku katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Kwa sehemu kubwa maandamano hayo yanaongozwa na makundi ya wanafunzi wanaompinga kiongozi wa zamani wa kijeshi ambaye sasa ni Waziri Mkuu, Prayut Chan Ocha na kundi lake linalomuunga mkono.

Jana waandamanaji wanaodai mageuzi makubwa ya demokrasia walifurika katika mnara wa demokrasia katikati ya mji wa Bangkok, uliojengwa kama ishara ya kumbukumbu ya mapinduzi ya mwaka 1932 yaliyokomesha utawala wa kiimla.

Waandamanaji hao walionekana wakipaza sauti wakisema: "Tunaung´oa udikteta".

Katika maandamano hao watu hao wakiwa wamebeba wamebeba mabango yenye kuipinga serikali ya Prayut na wengine walibeba vishada vilivyochongwa kwa mfano wa njiwa kama ishara ya amani.

Mivutano imeongezeka nchini Thailand katika kipindi cha wiki mbili zilizopita baada ya mamlaka za nchi hiyo kuwakamata wanaharakati watatu wa upinzani.

Wanaharakati hao walifunguliwa mashtaka ya uchochezi na kukiuka masharti ya kupambana na janga la virusi vya corona kabla ya baadaye kuachiwa kwa dhamana.

Wanaharakati hao waliamriwa kutorudia makosa waliyotuhumiwa kutenda, lakini mmoja wao ambaye ni kiongozi mashuhuri wa wanafunzi, Parit Chiwarak, amepuuza amri hiyo na kushiriki maandamano ambayo yalitokea jana.

Tarifa zaidi zinaeleza kuwa maandamano hayo yalifanyika sehemu mbalimbali na yalikuwa kama mfano wa vuguvugu la demokrasia la mjini Hong Kong.

Waandamanaji hao walidai mikusanyiko inayofanywa haina kiongozi maalum na kwa sehemu kubwa inatumia miito inayotolewa kupitia mitandao ya kijamii. **DW**

# BRUYNE: CITY BADO HAIJAWA VIZURI



**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne amesema Manchester City "inahitaji kujifunza" baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

City walikuwa wakipewa nafasi kubwa ya kushinda michuano hiyo msimu huu kueleka robo fainali mjini Lisbon, lakini walitolewa na Lyon Jumamosi kwa kichapo cha mabao 3-1.

Hi ni mara ya tatu mfululizo kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kikitolewa hatua ya robo fainali ya mashindano hayo.

De Bruyne aliisawazishia City baada ya Maxwel Cornet kufunga la kwanza kipindi cha kwanza, lakini Moussa Dembele alifunga mara mbili kuwapa ushindi huo Lyon ambao wametinga nusu fainali.

Baada ya mchezo huo, De Bruyne aliiambia BT Sport: "Tunahitaji kujifunza. Hatuko vizuri. Huo ndio ukweli."

Aliongeza: "Ni mwaka tofauti, wachezaji wale wale. Nafikiri kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri kwetu, nafikiri tunajua hilo.

"Tulianza taratibu. Hatukuwa na chaguo lolote, lakini kipindi cha pili tulicheza vizuri."

# Msimu mpya Bundesliga kuchezwa bila ya mashabiki

**MUNICH,** Ujerumani

MATUMAINI ya klabu za soka zinazoshiriki Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kuruhusu mashabiki wao kurejea kwa uchache viwanjani wakati msimu mpya wa ligi hiyo utakapoanza Septemba 18, mwaka huu, yameyeyuka.

Klabu 36 katika ligi kubwa mbili za juu nchini Ujerumani zilikubaliana vipengele vinne vya mapendekezo kutoka katika Bodi ya Ligi (DFL), ambavyo vingewezesha kuona mashabiki wakirejea viwanjani licha ya kuwapo kwa mlipuko wa virusi vya corona.

Klabu zilikubaliana kuuza tiketi za kibinafsi kwa ajili ya kufuatilia watazamaji, na hakuna mashabiki kutoka timu pinzani kwa mwaka 2020, hakuna pombe iliyoruhusiwa hadi Oktoba na mashabiki wakiwa wameketi tu kwenye viti.

Hata hivyo, makubaliano hayo lazima kwanza yapitishwe na serikali ya Ujerumani.

Mwanasiasa Dilek Kalayci, ambaye ni mwenyekiti wa mkutano wa mawaziri wa afya wa Ujerumani waliokutana Jumatatu, alimwaga maji baridi kwenye tumaini hilo.

"Hatupo tayari kupitisha maamuzi juu ya hayo kwa sasa," Kalayci aliliambia gazeti la Berliner Morgenpost kabla ya mkutano.

Aliongeza: "Soka la kulipwa halipo katika orodha ya vipaumbele vya kwanza kwa mawaziri wa afya."



# *Garcia awapa wakati mgumu Barcelona*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Barcelona imeonyesha kwamba, haina uwezo wa kutoa euro milioni 27 ili kumsajili mlinzi wa Manchester City, Eric Garcia.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 19, amekuwa akipewa nafasi ya kucheza mara kwa mara na kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, na ameonyesha kuwa na uwezo mkubwa kisoka, lakini hadi sasa amegoma kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuwatumikia matajiri hao wa jijini Manchester.

Maamuzi ya kugoma kusaini mkataba mpya, yameifanya Barcelona kuhitaji kumrejesha nyumbani kinda huyo, lakini ada ya kumng'oa pale Etihad imekua changamoto kwao.

Wakati Man City wakitajwa kuwa wanahitaji euro milioni 27 kumuachia nyota huyo, Barcelona wamesema wapo tayari kulipa nusu ya gharama hiyo iliyotajwa.

Guardiola ameshathibitisha kuwa nyota huyo anataka kuondoka klabuni hapo, lakini uongozi wa Man City unahitaji kuepuka kumuachia aondoke kama mchezaji huru msimu ujao, hivyo watahitaji kutazama tena mpango wao.

# Man City yamwania Messi

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Manchester City ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili nahodha wa Barcelona, Lionel Messi kama ataondoka klabu hapo, kwa mujibu wa gazeti la Mirror.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa akitajwa kwamba anaweza kuondoka pale Barcelona kipindi hiki cha majira ya joto.

Miamba hao wa Catalunya walitolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kichapo cha aibu cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich.

Kipigo hicho kimeibua uvumi kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa Messi kuondoka katika klabu hiyo ili kwenda kutafuta changamoto mpya.

Kocha, Quique Setien anatarajiwa kufukuzwa wakati wowote, huku majaliwa ya Messi yakipamba vyombo vya habari.

Messi mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake na Barca unamalizika msimu ujao na ameripotiwa kwamba yupo tayati kuondoka.

Klabu ya Man City mara kadhaa imekuwa ikihusishwa na kuwania kutaka kumsajili mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, huku Inter Milan nayo ikitajwa kuwa inamwania.





# HERRERA: PSG LAZIMA IBEBE UBINGWA UEFA

**PARIS,** Ufaransa

ANDER Herrera amesisitiza "yatakuwa makosa makubwa" kama Paris Saint-Germain haitabeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

PSG ilitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 1994-95.

Michuano hiyo imekuwa migumu kwa klabu hiyo ya Ligue 1 na sasa wamiliki wake Kampuni ya Qatar Sports Investments wana matumaini makubwa ya kulibeba taji hilo msimu huu.

Lakini wakati wachambuzi wengi wa soka wakiipa PSG nafasi kubwa ya kubeba taji hilo, Herrera anaona kwamba wakishindwa kulinyanyua yatakuwa makosa makubwa kwao.

"Kama tukishindwa kubeba taji la Ligi ya Mabingwa msimu huu, tutakuwa tumefeli sana," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumefanya kila kitu, hivyo tunatakiwa kuhakikisha kwamba tunatwaa taji hili msimu huu.

# *Barcelona inahitaji mabadiliko - De Jong*

**BARCELONA,** Hispania

FRENKIE de Jong amesema kichapo cha kutia aibu cha Barcelona cha mabao 8-2 kutoka Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kimeonyesha kwamba miamba hao wa LaLiga wana matatizo mengi.

Barca walikung'utwa bao nane kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1946 na miamba hao wa Hispania walitolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Lisbon, Ijumaa.

Na baada ya kichapo hicho kiungo De Jong amesema; "Nafikiri kipigo hiki kimeonyesha matatizo mengi yaliyopo ndani ya timu yetu."

De Jong ambaye ni msimu wake wa kwanza pale Camp Nou baada ya kutua akitokea Ajax, aliongeza kusema. "Nafikiri tulionyesha kwamba tunahitaji kufanya mabadiliko makubwa.

"Ni wakati mgumu kwa mashabiki, lakini kunahitajika mabadiliko makubwa sana ndani ya timu yetu.

"Tuliamini kwamba tunaweza kuifunga Bayern. Dakika 15 hadi 20 za kwanza walifunga haraka na tukasawazisha, lakini baadaye mambo yakawa magumu sana kwetu.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# OZIL SASA AFUNGUKA KUKATWA MSHAHARA

●●● Kwa yeyote ambaye angekuwa kwenye hali hii, ana haki ya kujua kila kitu, kujua...

**LONDON,** England

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil amefunguka kuhusu sakata lake la kugoma kupunguziwa mshahara kama sehemu ya kuendana na madhara ya mlipuko wa virusi vya corona.

**Klabu kadhaa zilipendekeza wachezaji wake kupunguziwa mishahara ili waweze kukidhi mahitaji ya kifedha ya uendeshaji wa timu hizo na Arsenal ni moja ya timu iliyopendekeza na kutekeleza utaratibu huo.**

Mengi yalizungumzwa kuhusiana na Ozil kugoma kupunguziwa mshahara wake, lakini taarifa kutoka kwa Ozil mwenyewe hazikusikika sana.

Ozil amefunguka kuhusu sakata hilo na ameliongelea kwa ufupi sana akijilenga yeye mwenyewe na kile alichodai ni kulazimishwa kwa wachezaji kufanya maamuzi bila kushirikishwa ipasavyo.

Akizungumza na gazeti la Athletics, Ozil alisema, "Kama wachezaji, tulitaka kuchangia, lakini tulihitaji taarifa zaidi na tulikuwa na maswali mengi ambayo hayakujibiwa.

"Ningekuwa tayari kuchukua hisa kubwa na pengine kukatwa mshahara kama ilipaswa kuwa hivyo mpaka pale mpira na hali ya kiuchumi ikiwa sawa. Lakini tulilazimishwa kufikia uamuzi huo bila ya kuwa na majadiliano thabiti.

"Kwa yeyote ambaye angekuwa kwenye hali hii, ana haki ya kujua kila kitu, kujua kinachofanyika na ni wapi fedha inakwenda.

"Hatukupewa taarifa za kutosha, tulielekezwa kufanya maamuzi tu. Ilikuwa ni mapema mno kwa kitu ambacho kilikuwa ni muhimu na chenye msukumo mkubwa."

Ozil alitajwa kama mchezaji pekee wa Arsenal aliyekataa kupunguziwa mshahara katika kikosi hicho.

Juma lililopita, Arsenal walitangaza azimio la kupunguza wafanyakazi 55 na inasemekana wachezaji wamekasirishwa na azimio hilo.

## ZISIKUPITE

### UNITED WAMTAKA NIGUEZ

KLABU ya Manchester United iko tayari kutoa ofa kwa kiungo wa kati wa Hispania, Saul Niguez,25, anayesemekana kuwa thamani yake ni pauni milioni 70 kutoka Atletico Madrid msimu huu. ***(Star)***

### RONALDO AMTAKA JIMENES

CRISTIANO Ronaldo anataka Juventus imsajili mchezaji wa kimataifa wa Mexico, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29, kutoka Wolves. ***(Gazzetta dello Sport, via Express)***

### SETIEN KUFUKUZWA BARCA

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien huenda akafukuzwa ndani ya siku chache zijazo, huku Mauricio Pochettino, Xavi na Ronald Koeman wakipewa nafasi ya kurithi mikoba yake pale Nou Camp. ***(Mundo Deportivo, in Spanish)***

### POGBA, DYBALA KUPISHANA

MANCHESTER United inafikiria makubaliano ya mabadilishano kati ya Paul Pogba, 27, na mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala, 26. ***(Tuttosport)***

### OBLAK SASA ANUKIA CHELSEA

MATUMAINI ya Chelsea kumsajili mlinda lango wa Atletico Madrid, Jan Oblak, 27, yameimarika huku klabu hiyo ya La Liga ikisemekana kuwa makini kutafuta mbadala wa kipa huyo wa Slovenia. ***(Football London)***

### CITY YAJIPANGA KWA WINKS

KLABU ya Manchester City inatayarisha kitita cha pauni milioni 40 kumsaka kiungo wa kati wa England na Tottenham, Harry Winks, 24. ***(Sun)***

### ARSENAL HAIPOI KWA PARTEY

ARSENAL ipo tayari kuimarisha kikosi chake kwa kumsajili Thomas Partey, 27, kutoka Atletico Madrid. ***(Star)***

### IGHALO AIPOTEZEA PSG

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Odion Ighalo mwenye umri wa miaka 31, hana nia ya kujiunga na Paris St-Germain licha ya taarifa kwamba klabu hiyo ya Ufaransa ina lengo la kumsajili raia huyo wa Nigeria, ambaye yuko kwa mkopo Old Trafford akitokea Shanghai Shenhua. ***(Manchester Evening News)***

### CHELSEA KUTOA KEPA

CHELSEA huenda ikamtoa golikipa wake, Kepa Arrizabalaga kwa Atletico kama sehemu ya mabadilishano ya kumpata, Jan Oblak kwa sababu haiko tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 100 ambayo ni bei ya nyota huyo. ***(Star)***

### YAGOMA KUMUUZA GABRIEL

KLABU ya Lille imekataa ofa ya euro milioni 20 kutoka kwa Everton kwa ajili ya kumsajili mlinzi wake, Gabriel mwenye umri wa miaka 22, kwa sababu wana makubaliano ya kumuuza mchezaji huyo kwa Napoli. ***(Gianluca di Marzio)***

### N'CASTLE YAMWANIA SMALLING

KLABU ya Newcastle inanyatia kumsajili mlinzi wa Manchester United, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, ambaye msimu uliopita alikuwa Roma kwa mkopo na pia analengwa na klabu yake ya zamani, Fulham. ***(Newcastle Chronicle)***

HABARI MICHEZO

## Kipa wa Uganda atua Simba Queens

**Na Saada Akida**

KIPA namba moja wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Uganda, Ruth Ataro, yupo mbioni kusaini mkataba wa kutumikia Simba Queens iliyopo sokoni kuimarisha kikosi chake ikiwa na lengo la kutetea ubingwa wao kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu ya Wanawake.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mratibu wa timu hiyo, Selemani Erasssy, alisema tayari wamefanya mazungumzo na kipa huyo ambaye amekubali ofa ya Simba.

Alisema baada ya kutuma ofa yao kwa kipa huyo, ameridhia na anatarajiwa kuwasili nchini na kusaini mkataba wa kukitumikia kikosi cha timu yao hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake.

"Kila kitu kuhusu mchezaji huyo kinaenda vizuri tunatarajia wiki hii atakuja nchini kwa ajili ya kusaini pamoja na kuwa miongoni mwa wachezaji watakaotambulishwa katika Sherehe za 'Simba Day," alisema Erassy.

Alisema pia wako katika mchakato wa kusajili wachezaji wawili wa ndani ambao hakutaka kuwaweka wazi kwa madai kuwa kuna baadhi ya timu wanahitaji huduma za nyota hao.

"Hatufanyi usajili mkubwa ukizingatia kwa wachezaji wa ndani viwango vinalingana, pia kwetu tulikuwa tunahitaji kipa mwenye uzoefu mkubwa wa michuano ya kimataifa hali ambayo tumerudi kwa mara nyingine kwa Aturo ambaye msimu uliopita ilishindikana kumpata kwa sababu alikuwa anasoma chuo," alisema Erassy.

## Idumu FC yakata tamaa kupanda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Idumu FC inayocheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja imesema haina matumaini makubwa ya kupanda daraja msimu huu kwa kuwa ligi hiyo inaushindani na timu moja tu ndiyo itakayopanda Ligi Kuu.

Timu ya Idumu FC ipo nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ikiwa na alama 35 tayari ikicheza michezo 20, kabla ya mechi ya jana.

Akizungumza na gazeti hili wiki iliyopita, Katibu wa timu hiyo, Mtumwa Mabrouk, alisema timu zote zilizopo katika nafasi za tatu bora zinapigania kupanda daraja hali inayosababisha ligi hiyo kuonekana kuwa ngumu kwa kila timu wanayocheza nayo.

Alisema licha ya timu kubakisha michezo michache kumaliza msimu, hakuna ambayo imejihakikishia kupanda daraja na hii inatokana na ushindani uliopo katika ligi hiyo.

"Ligi ngumu sana, timu zote zinaushindani wa hali ya juu, ambazo zipo katika tatu bora zote ukishukanazo dimbani mchezo unakuwa mgumu sana na lolote linaweza kutokea, hivyo Idumu tunachoangalia zaidi ni kulinda daraja endapo ikitokea kupata nafasi ya kupanda basi tutapanda daraja," alisema.

Kinara wa ligi hiyo ni timu ya Black Sailor yenye alama 41.

# YANGA NA 'SIZITAKI MBICHI' KWA NIYONZIMA, BWALYA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya awali kushuhudia kiungo Ally Niyonzima akitua Azam FC na juzi mchezaji mwingine wa nafasi hiyo, Larry Bwalya akijiunga na Simba, licha ya wote wawili kuhusishwa na Yanga, klabu hiyo imesema wala haikuwahi kuwahitaji viungo hao wanyumbulifu dimbani.

**Aidha, Yanga imesema wapinzani wao wa jadi, Simba wanafanya siasa za kutaka kuwaridhisha wanachama na mashabiki wao baada ya kuwazidi kete kwenye usajili wa Bakari Mwamnyeto na kumchukua Ofisa Mtendaji wao, Senzo Mazingisa.**

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli amesema hawakuwa na nia kabisa ya kuwataka wachezaji hao na wala wazo la kumsajili mchezaji huyo, lakini wanachofanya Simba kwa sasa ni kuwafariji wanachama na mashabiki wao ili waone kuwa usajili wao ni wa kuipiga bao Yanga.

"Si kama huyo mchezaji waliyemsajili ni mbaya, lakini si kila mchezaji analetwa Yanga basi sisi tunamtaka, sisi tunaangalia tunataka nani na kwa wakati gani. Mashabiki na wanachama wa Yanga waelewe kuwa sisi tuna malengo yetu na wachezaji wetu tunaowahitaji, si hawa wanaowasajili, tukishindana nao wenzetu huwa hawafui dafu," alisema Bumbuli.

Alisema anachofahamu yeye ni kwamba walishindana na Simba sehemu mbili tu, ya kumuwania Mwamnyeto na Senzo tu.

"Kwanza ilikuwa ni ya Mwamnyeto, tumeshinda, ya pili ni ya Senzo nayo tumewakata maini, sasa hii yote inayofanyika ni kutaka kujifariji na kuwatuliza wanachama na mashabiki wao," alisema.

Bumbuli alisema katika kipindi hiki cha usajili kuna baadhi ya mawakala wamekuwa na tabia ya kutengeneza habari ili ionekane wao wanamtaka, kitu ambacho kinasababisha wenzao kukimbilia kuwasajili bila kufanya utafiti kwanza.

"Hata yule aliyesajiliwa na Azam, Ally Niyonzima hatukumtaka, unajua tumeletewa majina ya wachezaji zaidi ya 1,000 na mawakala, sasa unaangalia nani atakufaa na kwa nafasi gani, siyo kila mchezaji usajili, lakini kuna tabia ya mawakala wanakuletea video ya mchezaji, anakutumia halafu mnaongea au kuchati, maongezi anayapeleka kwa wengine ili kuonyesha kuwa viongozi wa Yanga wanamhitaji, basi kuna watu wanakurupuka tu na kwenda kusajili," Bumbuli alizidi kusisitiza.

Kuhusu usajili, Bumbuli alisema wanafanya usajili wa uhakika na kuwataka Wanayanga wavute subira na kutosikiliza maneno ya propaganda.

Kwenye suala la kocha, alisema watakayemleta hatokuwa mgeni kwenye mazingira ya Tanzania na wachezaji wa kibongo pia.

KITITA...




Mshindi wa mechi 12 kati ya 13 za Jackpot ya SportPesa, Ostan Mgaya (45), mkazi wa Lindi Mjini akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 21.7 ambayo amekabidhiwa jijini Dar es Salaam juzi. Jackpot ya SportPesa kwa sasa imefika Sh. 222,415,400. **PICHA: SPORTPESA**

# *Namungo yamnasa beki wa Yanga*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo imeendelea na mkakati wake wa kukitengeneza kikosi chake kwa ajili ya Ligi Kuu msimu ujao wa 2020/21 na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF) kwa kumsajili aliyekuwa beki wa kushoto wa Yanga, Jaffar Mohamed.

Jaffar, ametambulishwa kwenye mtandao rasmi wa klabu hiyo ambao pia umeeleza viongozi wa klabu hiyo wanafuraha kukamilisha usajili wa mchezaji Jaffar Mohamed Mbena kwa mkataba wa mwaka mmoja.

Mchezaji huyo ambaye alisajiliwa na Yanga miaka miwili iliyopita akitokea Majimaji ya Songea, msimu huu amemaliza mkataba wake na klabu hiyo, ambayo ilionekana haikuwa na nia ya kutaka kuendelea naye.

Jaffar anakuwa ni mchezaji wa tano mpya kusajiliwa na Namungo FC yenye maskani yake Ruangwa mkoani Lindi.

Wengine ambao mpaka sasa wamesajiliwa ni Abdulhalim Humud kutoka Mtibwa Sugar, Steven Sey, Mghana aliyekuwa akichezea Singida United, Fred Tangalo kutoka Lipuli na Sixtus Sabilo akisajiliwa kutoka Polisi Tanzania.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu alisema wanatarajia kuingia mkataba na Kocha Mkuu, Hitimana Thiery baada ya kurejea nchini akitokea kwao alikokwenda kwenye msiba wa mdogo wake.

"Tulikuwa tuingie naye mkataba, lakini haikuwezekana kwa sababu alipata msiba, isingewezekana akae na sisi kuzungumzia masuala ya mkataba wakati amefiwa, hivyo tukaona kwanza aende akahudhurie mazishi kwanza, halafu akirudi atakuwa ametulia, lakini kila kitu kiko vizuri," alisema Zidadu.

# Michezo

Jumatatu Agosti 17, 2020

Nipashe




Ozil sasa afunguka kukatwa mshahara

UKURASA 22

MTAMBO WA MABAO...




Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola (kushoto), akimkabidhi mkataba mshambuliaji mpya wa timu hiyo raia wa DR Congo, Chris Mugalu, ambaye jana alitia saini kuitumikia kwa miaka miwili. **PICHA: SIMBA**

## Wachezaji tisa bora namba 9

**LONDON,** England

NAMBA ya jezi imekuwa na maana kubwa mno kwa kumtambulisha...




HABARI UK. 12

## Yanga yatoa neno Niyonzima, Bwalya

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya awali kushuhudia kiungo Ally Niyonzima akitua Azam FC na juzi mchezaji mwingine wa nafasi hiyo...

HABARI UK. 23

# SIMBA: USAJILI HUU NI WA MABINGWA AFRIKA

## Mugalu amwaga wino, Micho makocha DR Congo wasema ni mtambo wa mabao...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaimarisha kikosi cha timu yao kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Simba imezidi kujijenga kwa kuingia mkataba wa miaka miwili na mshambuliaji Mkongomani Chris Mugalu kutoka Lusaka Dynamos ya Zambia.

**Kutua kwa Mugalu kunazidi kuimarisha safu ya ushambuliaji ya Simba na haitamchukua muda straika huyo kutengeneza uelewano mzuri kwani aliwahi kucheza pamoja na Clatous Chama katika kikosi cha Power Dynamos mwaka 2017.**

Mugalu anakuwa mchezaji wa nne wa kimataifa kusajiliwa Simba msimu huu na wa sita kwa ujumla kwa wachezaji wote waliosajiliwa na klabu hiyo tangu dirisha la usajili lilipofunguliwa Agosti Mosi, mwaka huu.

Wachezaji wengine wakimataifa waliosajiliwa na Simba ni pamoja winga Mghana Bernard Morrison (mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Yanga), beki wa kati Mkenya Joash Onyango ambaye ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake wa Gor Mahia ya kwao Kenya na straika Mzambia Larry Bwalya kutoka Lusaka Dynamos.

Kwa upande wa wachezaji wa ndani ni beki wa kati Ibrahim Ame aliyetokea Coastal Union ya Tanga, David Kameta 'Duchu' (Lipuli FC)na Charles Ilamfya kutoka KMC FC.

Mugalu alitua nchini juzi akiwa na wakala wake Paricha Chikoye, ambaye ndiye alimleta Bwalya na Chama na kwenda moja kwa moja kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi Simba, Mohammed "Mo" Dewji na kukubaliana kusaini mkataba wa miaka miwili kabla ya jana kutambulishwa rasmi.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Simba kupitia mtandao wao wa kijamii wa Instagram zilieleza: "Scout wa Simba, benchi letu la ufundi, makocha wa Zambia na Congo wote wamekubaliana kwamba kama Simba inataka kupigania taji la ubingwa wa Afrika ni lazima iwe na mshambuliaji mwenye uwezo kama Chris Mugalu.

"Kocha Micho (Milutin Sredojevic)ambaye ni kocha wa timu ya Taifa ya Zambia kwa sasa aliposikia tunamsajili Chris, alisema sasa Simba inakwenda kufanya kitu Afrika.

"Ni mshambuliaji wa viwango vya juu katika ukanda huu wa Afrika. Ni 'killer' ni 'bull' ni 'animal" nje na ndani ya boksi. Nadhani mtaelewa 'focus' (malengo) yetu. Una (John) Bocco, una (Meddie) Kagere na una Mugalu kwa hapa nyumbani mtatusamehe tu wenzetu katika ushindani."

Naye Katibu Mkuu wa Simba, Anord Kashembe alisema: "Mashabiki na wanachama wanatakiwa kutulia, viongozi wanafanya usajili wa wachezaji kulingana na mapendekezo ya kocha pia mahitaji ya timu yetu, kwa msimu huu tunataka kucheza fainali ya Ligi ya Mabigwa," alisema Kashembe.

Alisema kikosi chao kinatarajia kuanzia mazoezi leo katika Uwanja wa Mo Simba Arena chini ya Kocha Mkuu Sven Vandenbroeck ambaye aliwasili nchini jana akitokea kwao Ubelgiji kwa mapumziko mafupi.

Kashembe alisema wameona makosa yao ya msimu uliopita katika michuano hiyo na sasa wamefanyia kazi ikiwamo suala la usajili katika nafasi ya beki wa kati na ushambuliaji.

Alisema mbali na usajili huo pia malengo makubwa ni kufanya maboresho madogo katika kikosi pamoja na kumwongezea mkataba Sven.

"Baadhi ya wachezaji wetu waliokwenda likizo wanatarajia kurejea ndani ya siku hizi mbili, kuingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mechi yetu ya Ngao ya Jamii na msimu mpya wa ligi unaotarajia kuanza hivi karibuni, Sven ataendelea kuwa kocha wetu, hatuwezi kumuacha," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >